BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

Simu ya Upepo: Baraza
Nambari ya Simu:2230234/5
Tele Fax. Nam. (024)2230215

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR

KAMATI YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAMATI YA MIFUGO,UTALII, UWEZESHAJI NA HABARI

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

SEHEMU YA KWANZA

1.1 UTANGULIZI

Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 104(h) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi-Zanzibar, Toleo la mwaka 2011. Majukumu na kazi za Kamati hii yameainishwa katika kanuni ya 113 ya Kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi ambapo, pamoja na mambo mengine, Kamati ina majukumu ya msingi yafuatayo:

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.

c) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, ambayo kwenye taarifa hii itatajwa kama “Kamati” inawajibika kuzisimamia Wizara tatu za Serikali zifuatazo:

1. Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
2. Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na Ushirika
3. Wizara ya Mifugo na Uvuvi

1.2 WAJUMBE WA KAMATI

Kamati ina Wajumbe wanane na Makatibu wawili, kama ifuatavyo:

1. Mhe. Asha Bakari Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Mohammed Said Mohamed - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Assaa Othman Hamad - Mjumbe
4. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
5. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Abdi Mosi Kombo - Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
8. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe
9. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
10. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

1.3 UTARATIBU WA KAZI

Kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita, kati ya Unguja na Pemba kama ifuatavyo:

- Kuanzia tarehe 19/09/2011 hadi tarehe 30/09/2011, kwa upande wa Unguja.
- Tarehe 12/12/2011 hadi tarehe 23/12/2011, huko Pemba.
- Tarehe 20/02/2012 hadi tarehe 02/03/2012 Unguja.

1.4 MPANGILIO WA TAARIFA

Ripoti hii imegawika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi na inajumuisha utangulizi wenyewe, Wajumbe wa Kamati pamoja na mpangilio wa kazi. Sehemu ya Pili inahusu utekelezaji halisi wa majukumu ya Waizara ya Habarí, Utamaduni, Utalii na Michezo. Sehemu ya tatu inaelezea utendaji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Sehemu ya nne inahusu utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika pamoja na Maoni ya Kamati kwa ujumla.

SEHEMU YA PILI
WIZARA YA HABARI UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO.

2.1 UTANGULIZI

Wizara hii inajumuisha vitengo mbalimbali katika kufanikisha majukumu yake kwa Unguja na Pemba. Vitengo hivyo ni kama vifuatavyo:-

- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
- Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC)
- Idara ya Habari Maelezo
- Shirika la Magazeti ya Serikali
- Bodi ya Sensa ya filamu na sanaa za maonesho
- Idara ya Makumbusho na mambo ya Kale
- Kamisheni ya Utalii
- Baraza la Taifa la Michezo.

- Idara ya Uendeshaji na Utumushi
- Tume ya Utangazaji
- Chuo cha Uandishi wa Habari
- Kamisheni ya Utamaduni na Michezo
- Baraza laKiswahili
- Baraza la Sanaa
- Shirika la Utalii
- Chuo cha Maendeleo ya Utalii
- Hoteli ya Bwawani

Wizara hii imeundwa kwa madhumuni ya kusimamia na kuratibu sekta kuu nne (4) ambazo ni Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Malengo yote yaliyopangwa yametekelezwa kwa wastani wa asilimia 70 na 80 ya matarajio isipokuwa baadhi ya malengo tu ambayo hadi hivi sasa hayajatekelezwa. Sababu kuu za kushindwa kutekelezwa malengo hayo ni kutokana na ufinyu wa Bajeti ambayo Wizara imetengewa kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

2.2 UTEKELEZAJI WA WIZARA - UNGUJA

Kamati ilipata fursa ya kukagua utendaji halisi wa majukumu ya msingi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kama ifuatavyo:

2.2.1 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

- **Uimarishaji wa miundombinu na kuongeza ufanisi kazini**

Idara imelifanyia matengenezo madogo madogo jengo la Wizara ili kuliweka katika hali ya kupendeza na kuvutia. Aidha, ununuzi wa samani mbali mbali za kiofisi umefanywa na samani zilizonunuliwa ni kama vile, meza, viti kwa matumizi ya wafanyakazi na kufanya kazi kwa ufanisi. Kulipia gharama za kodi ya nyumba ambazo zinatumika kwa kuwaweka makocha wa michezo wa nje ya nchi.

Katika kukuza michezo na kuwafanya wafanyakazi wa Wizara kuipenda michezo, Idara imefanikiwa kuzilipia gharama za maandalizi ya timu hiyo ya Wizara ili kuweza kushiriki katika mashindano ya ndani na yale ya Tanzania Bara. Idara imelipa gharama za ununuzi wa mashine, Kompyuta, Friji na Vespa.

- **Elimu kwa wafanyakazi**

Hadi kufikia Disemba 2011, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeweza kuwalipia gharama za masomo wafanyakazi sita (6) wanaojiendeleza katika fani mbali mbali nchini.Rasilimali watu (2) Ngazi ya Stashahada, Watu wawili (2) Shahada ya kwanza na Shahada ya Pili watu wawili (2).

2.2.2 IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Majukumu ya idara hii ni kuandaa sera na mipango ya maendeleo ya Wizara na kusimamia utekelezaji wake, pamoja na kusimamia udhibiti wa bajeti ya Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

- **Kuimarisha shughuli za Mipango, Sera na Utafiti**

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeshiriki kikamilifu katika utafiti unaoendeshwa na Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho. Utafiti huo unazungumzia juu ya Maadili ya Mzanzibari. Aidha Idara imefanya upembuzi katika uwanja wa Mao Tse Toung juu ya matumizi ya kisasa ya michezo na matumizi mengineyo. Utafiti huu ni muhimu kwa maendeleo ya michezo na Taifa.

- **Kusimamia utekelezaji wa sera na matokeo ya tafiti**

Idara Imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Maafisa Mipango wote wa Wizara kwa upande wa Unguja ili kuimarisha utendaji wa kazi zao za kila siku.

- **Mapambano dhidi ya virusi vya UKIMWI**

Wizara imo katika utaratibu wa kutayarisha Mpango Mkakati wa Ukimwi (AIDS Strategic Plan) ya miaka mitano (5).

2.2.3 SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA ZANZIBAR (ZBC)

- **Uundwaji wa Bodi ya Shirika la Utangazaji**

Utaratibu wa uundaji wa bodi ya Shirika la Utangazaji unaendelea na kwa hivi sasa legal notice tayari imeshatiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar.

- **Ununuzi wa vifaa**

Kwa kipindi cha Julai/Disemba 2011, Wizara imefanikiwa kununua Viyoyozi (Air Condition) viwili kwa matumizi ya kituo cha kurushia matangazo Chumbuni. Baada ya kuhamishwa mitambo kituoni hapo, viyoyozi hivyo vitatumika kwenye sehemu mpya iliyopelekwa mitambo hiyo ambapo ni Bungi.

Ili kuwa na utendaji mzuri wa kazi na kuziimarisha Ofisi za Shirika la Utangazaji (ZBC), Shirika limenunua kompyuta na vifaa vyake kwa lengo la kurahisisha kazi. Kubadilisha vifaa vya kurikodia vya Shirika la Utangazaji (ZBC) vyenye kutumia teknolojia ya analojia na kuviweka katika mfumo wa dijitali.

- **Uhifadhi wa nyaraka kwa njia za kisasa**

Shirika limefanikiwa kuhamisha kumbukumbu zote za nyimbo na hotuba za waheshimiwa kutoka kwenye kanda na kuzihifadhi kwenye mfumo wa sahani (CD) na kompyuta.

- **Urushaji wa vipindi na matayarisho ya kuingia kwenye teknolojia ya dijitali**

Shirika la Utangazaji (ZBC) limefanikiwa kufunga mitambo mipya na ya kisasa (transmeter) ya aina ya dijitali huko Pemba. Hadi kufikia mwezi Disemba 2011, Kamati iliarifiwa kwamba mitambo hiyo haijaanza kazi ya kurusha matangazo ya digitali kutokana na kutokamilika kwa matayarisho yake.
Aidha, ZBC inatarajia kuanzisha utaratibu wa kupasha habari kwa njia ya ishara ili kuwapatia fursa ya kupata habari watu wenye mahitaji maalum. (Wasiosikia na wasioweza kusema).
Katika kufanya matangazo ya televisheni yapatikane bila ya usumbufu, Shirika limefanikiwa kuuteremsha mnara wa masafa ya kati kutoka Chumbuni kwenda katika eneo la Bungi. Eneo la Chumbuni linatarajiwa kutumika kwa matumizi mengine ya maendeleo ya nchi.

2.2.4 IDARA YA HABARI MAELEZO

Idara imeweza kuimarisha uwezo wa waandishi wa Habari na wafanyakazi kwa kuimarisha Sekta ya Habari nchini kwa kutoa taarifa tofauti za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Halkadhalika, idara imeweza kukuza usambazaji wa habari za maendeleo mjini na vijijini kwa kutumia Gari la Sinema, zikiwemo kupunguza umaskini na maambukizi ya Ukimwi, jinsia, mazingira na utumikishwaji wa watoto (child labour) katika kuimarisha upatikanaji na utoaji wa habari nchini.

- **Uimarishaji wa jengo la Idara na vitendea kazi**

Pamoja na kuendeleza shughuli za matengenezo ya Ofisi, Idara imenunua Vespa ili kurahisisha ufuatiliaji na utendaji kazi zake.
Aidha, Idara imenunua vifaa vya Ofisi kama Kompyuta, Mashine za kutolea kopi Mbili (2) Kamera 1 na Uninterruptible Power Supply (UPS) nne (4) ili kufanikisha utendajikazi wa Idara. Hata hivyo vifaa vya “Production” vya “Dark Room” “UPS”, “Fire Wire”, “Sound Card” na “Editing” pia vimenunuliwa.
Idara imenunua vipuri vya gari ya Ofisi na kugharamia malipo ya fundi.
Hatua za utekelezaji zinaendelea kwa kujenga maktaba ya picha.

2.2.5 SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI

Shirika la Magazeti ya Serikali limeimarisha usambazaji wake wa magazeti ndani na nje ya Zanzibar, ili kuweza kulitafutia soko zaidi na kuhakikisha kwamba Gazeti linawafikia wasomaji Zanzibar nzima na maeneo mengi zaidi ya Tanzania Bara.

Aidha, Shirika limeweza kulipa madeni ya uchapishaji magazeti kwa kampuni ya Multicolour na kampuni ya Monic Trust.

2.2.6 TUME YA UTANGAZAJI

Kwa kipindi cha Julai/Disemba 2011, Tume imefanikiwa kuratibu shughuli za Utangazaji nchini kwa kutoa huduma bora za utangazaji ili zisiingiliane baina ya watumiaji. Vile vile, Tume imeweza kujenga uelewa kwa vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya Watu binafsi juu ya maadili ya utangazaji kwani imebainika kuwa wengi kati ya wanahabari wapya hawajui maadili ya kazi zao.
Aidha, Tume imeandaa rasimu ya Sera ya Utangazaji kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapisha vipeperushi kuhusu taaluma ya utangangazi wa dijitali.

2.2.7 CHUO CHA UANDISHI WA HABARI

Kwa kipindi cha Julai/ Disemba 2011, chuo kimetekeleza yafuatayo:

1. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wake wawili (2) ili waweze kukidhi mahitaji ya Chuo.
2. Kununua vifaa tofauti vya kufundishia na zana za Ofisi ili kuweka mazingira mazuri ya kusomeshea.
3. Kufanya maandalizi ya kupata mshauri wa mafunzo ya mtaala wa Chuo, na kwa sasa Mpango Mkakati umefanyiwa mapitio ya mwisho.
4. Kuandaa "Prospectus na Brochures" za kukitangaza Chuo ambazo hadi kufikia Disemba, 2011 ziko katika hatua za mwisho.

2.2.8 KAMISHENI YA UTALII

Kwa kipindi cha Julai/disemba 2011, Kamisheni imeweza kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo :

1. Kamisheni imewalipia wafanyakazi wake walioko masomoni. Kwa ujumla kuna wafanyakazi wanane (8) ambao wanaendelea na masomo yao ndani na nje ya nchi katika ngazi za Cheti, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili (PhD). Aidha, mfanyakazi mmoja (1) alipatiwa mafunzo mafupi nchini Japan kuhusu Utalii Endelevu kwa nchi za Afrika (Sustainable Tourism Development in African Countries) katika kuhakikisha taaluma inapatikana kwa watendaji wa Kamisheni ya Utalii.

2. Katika kuimarisha uhusiano na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi, Kamisheni ya Utalii ilishiriki mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nchini Kenya na kuweza kuitangaza Zanzibar juu ya vivutio vyake kwa washiriki wa mkutano huo na dunia kwa ujumla. Aidha Kamisheni imeshiriki katika vikao mbali mbali vya mashirikiano na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

3. Kwa kushirikiana na Idara ya Takwimu, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii (Bara), Kamisheni imekamilisha ukusanyaji wa taarifa kwa mwaka 2011.

4. Vikundi vinne kutoka nchi za Sweeden, China (CBN), Uingereza (The Scottish Sun) na Malaysia (VAYA) vilipokelewa hapa Zanzibar.

5. Aidha kwa upande wa machapisho, Kamisheni imefanikiwa kuchapisha kalenda za ukutani, na jarida la Karibu Zanzibar vimechapishwa nakla 250.

6. Matangazo ya kitalii katika majarida ya kimataifa ya "a.c braby Commercial Directory", "Travel World China" na "Business Times" yametolewa kwa lengo la kuutangaza Utalii wa Zanzibar.

2.2.9 CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII

- Chuo kimefanya matengenezo ya jengo ili kupata sehemu nzuri ya kufundishia katika kuimarisha miundo mbinu ya chuo na kukipatia hadhi inayostahiki.

- Chuo pia kimeweza kuajiri Mshauri Elekezi wa kutayarisha Mpango Mkakati wa Chuo ili kiweze kwenda sambamba na mahitaji ya wadau mbali mbali.
- Aidha, chuo kimefanya warsha ya wafanyakazi kujadili Mpango Mkakati wa Chuo kwa mwaka 2011-2016.
- Vilevile chuo kimewagharamia walimu wawili (2) katika nafasi za kwenda kusoma Shahada ya Kwanza katika fani ya Utalii Open University, na mfanyakazi mmoja (1) amepatiwa Shahada ya Uzamili ya Uhasibu katika Chuo cha Uongozi wa Fedha, Chwaka.

2.2.1.1 SHIRIKA LA UTALII ZANZIBAR

Katika kuongeza utoaji wa huduma bora kwa watalii watakaoshughulikiwa na Shirika (Package Tourism), Shirika limefanya juhudi za kuwasiliana na kampuni mbili (2) za Kichina zinazojishughulisha na utembezaji wa watalii. Kampuni zenyewe ni Guanghoung Travel Services na Kampuni ya Travel Abroad Online, Kampuni hizi zimeshatiliana saini na Shirika kuleta watalii kwa makundi hapa Zanzibar kwa vile soko la watalii wa Kichina ni soko jipya hapa nchini.

2.2.1.2 HOTELI YA BWAWANI

Kwa kipindi cha Julai/Septemba 2011, Hoteli ya Bwawani imetekeleza yafuatayo:

- Kufanya ukarabati mkubwa wa vyumba kwa kuweka tiles, kuziba paa la Salama Hall na uchimbaji wa mitaro kuweka baadhi ya samani katika Hoteli ili kuweza kukidhi mahitaji ya wateja.
- Hoteli imeanza kufanya marekebisho ya tatizo la mmong'onyoko wa ardhi unaosababishwa na mawimbi makali ya bahari kwa kushirikiana na Shirika la bandari.

2.2.1.3 IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE

- Imefanya maonesho ya karne ya ishirini (20).
- Imetayarisha na kutoa matangazo mbali mbali katika Redio, TV, mitandao ya Intaneti na hata kwa waongozaji wageni (Tours Guide), juu ya Makumbusho na Historia ya Zanzibar ili kuweza kupata idadi kubwa ya wageni na kuongeza vyanzo vya mapato vya nchi.
- Imelifanyia matengenezo jengo la makumbusho la Hamamni Baths ili kulirudisha katika hadhi yake ya awali na kuwapata wageni wengi.

2.2.1.4 KAMISHENI YA UTAMADUNI NA MICHEZO

- Katika kukuza na kuinua vipaji vya wasanii wetu wa Zanzibar, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imeendesha semina mbili kati ya Unguja na Pemba kwa kuwaelimisha Wasanii hao umuhimu wa kazi zao kwa jamii, na kuendelea kuulinda na kuuthamini Utamaduni wetu wa Zanzibar
- Kamisheni imeendesha Tamasha la Utamaduni la Mzanzibari ambalo ni chachu kwa Wazanzibari ili kuweza kuulinda na kuuenzi Utamaduni wao.
- Pia, Kamisheni imeratibu na kushiriki kikamilifu katika Tamasha la Utamaduni la watu wa Oman lililofanyika hapa Zanzibar.

2.2.1.5 BODI YA SENSA YA FILAMU NA SANAA ZA MAONESHO

- Imehakiki Tamasha la "100% Zanzibar ili kuhakikisha kwamba maonesho wanayoyafanya hayakiuki Mila na Desturi za Mzanzibari pamoja na kukagua filamu na sanaa tofauti.
- Imefanya vikao vya kitaalamu vya utafiti juu ya dhana nzima ya Maadili ya Mzanzibari. Aidha Utafiti huo umefanywa kwa upande wa Unguja na Pemba hatua iliyobakia sasa ni kuingiza data kwa ajili ya kutayarisha kitabu.

2.2.1.6 BARAZA LA KISWAHILI

Kwa kipindi cha Julai/Septemba 2011, Baraza limetekeleza kazi zake kuu zifuatazo:

- Kufanya utafiti kwa baadhi ya wasanii wa zamani wa Zanzibar, ambao umeanza kufanyika ili kuweza kuutambua mchango wao katika Lugha yetu ya Kiswahili.

- Limelikamilisha Kamusi la Kipemba na kwa sasa lipo katika hatua ya machapisho huko Oxford Nairobi.

2.2.1.7 BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO

Kwa kipindi cha Julai/Disemba, Baraza limefanya yafuatayo:

i) Kuandaa mashindano ya Kombe la Urafiki la Mpira wa Miguu yaliyofanyika Pemba kwa kuzishirikisha timu nane (8). Aidha Baraza limeandaa bonanza kuu la mazoezi ya viungo kwa vyama vinavyoshiriki katika mazoezi hayo.

ii) Kuratibu mashindano ya Mpira wa Wavu huko Pemba ambapo timu nane (8) ziliweza kushiriki katika mashindano hayo.

iii) Vilevile, Baraza lilifanya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa vijana (Central League) yaliyofanyika Pemba kwa kuzishirikisha timu sita (6).

iv) Baraza limefanikisha mashindano ya mchezo wa hoki kwa chama cha hoki Zanzibar.

v) Kufanyika kwa semina elekezi juu ya sheria mpya ya BTMZ kwa viongozi wa mabaraza ya michezo ya Wilaya zote za Pemba.

vi) Kuandaa semina juu ya dhamana na wajibu wa viongozi wa michezo katika Wilaya tofauti za Unguja na Pemba, miongoni mwa Wilaya hizo ni: - Micheweni, Mkoani, Kusini na Kaskazini A

2.3 UTEKELEZAJI WA WIZARA KWA UPANDE WA PEMBA

Kwa kipindi cha Julai/Disemba, Ofisi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

i) Imekamilisha kazi ya uwekaji Nyasi Bandia katika uwanja wa Gombani Pemba. Uwekaji wa Nyasi hizo umefanywa na wataalamu kutoka kampuni ya Greenfield ya Uholanzi, na kwa sasa uwanja huo umeanza kutumika kwa mashindano ya michezo.

ii) Kazi ya ufungaji transmita mbili mpya za kisasa za kurushia matangazo ya TV imekamilika, kazi ambayo imewezesha upatikanaji wa matangazo ya TV ya Shirika la Utangazaji huko Pemba.

iii) Imetoa huduma ya Redio Micheweni kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata habari mbali mbali na burudani, kwa madhumuni ya kuongeza idadi ya wasikilizaji.

iv) Imelipia huduma za maji, umeme na '*internet*' kwa Idara na Taasisi zake zote, na kwamba huduma hizo zinapatikana kwa uhakika. Aidha uwepo wa huduma za '*internet*' zimewarahisishia waandishi wa Habari katika upokeaji na upelekaji wa Habari kwenye vyombo vya Habari.

v) Kupitia Shirika la Utangazaji (Redio) imerusha hewani vipindi 35 vya moja kwa moja na vipindi 70 vya kurikodiwa, vipindi hivyo vilihusu uokoaji wa zao la karafuu, kilimo cha mwani, uchumi, mazingira, biashara na ziara za viongozi wa Kitaifa.
Kikao cha pamoja cha wafanyakazi kuhusu Elimu ya Ukimwi na upimaji kwa hiari kimefanyika, kikao hicho kimewajumuisha wafanyakazi wote wa Ofisi Kuu Pemba.

vi) Imewalipia ada wafanyakazi wake saba (7) ambao wapo masomoni kwa ajili ya kukuza viwango vyao vya elimu katika ngazi ya cheti, kwa fani ya Masjala wawili (2), Manunuzi mmoja (1), Uhasibu wawili (2) na Mambo ya Utalii wawili (2).

vii) Kazi ya ujenzi inaendelea, kuzungushia uzio na ujenzi wa sehemu ya kuhifadhia jenereta eneo la Mnara zimefanyika katika wastani wa kuridhisha.

2.4 MATUMIZI YA FEDHA

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi 6, 257, 000,000/= kwa kazi za kawaida na jumla ya shilingi 2, 960, 000,000/= kwa kazi za maendeleo na makusanyo ya shilingi 1, 212, 800,000/= kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali.

Hadi kufikia mwezi Disemba 2011, Kamati imejulishwa kwamba, Wizara imeingiziwa jumla ya shilingi 2, 737, 045,841.50/=**.** Katika fedha hizo Mishahara ni 1, 070, 482,394/=, Ruzuku ni 789, 642,638/= na Matumizi Mengine (OC) ni 876, 920,810/=.

Aidha, jumla ya Shilingi 164, 069,440/= zimekusanywa na Wizara kwa kupitia taasisi zake na kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali.

2.5 CHANGAMOTO

1. Uchafu uliokithiri katika maeneo mbali mbali hususan maeneo ya mjini unazorotesha sekta ya utalii nchini. Baadhi ya watalii hulalamikia hali hiyo ambayo kwa upande wao wanaiona kuwa inawahatarishia maisha yao.

2. Kutokubalika ujenzi wa njia hata ile ya fusi katika msitu wa ngezi unarejesha nyuma maendeleo ya utalii Pemba kwani watalii hushindwa kufika mahoteli wanayoyataka kwa urahisi. Aidha, kutotengenezwa njia hiyo kunahatarisha usalama wa wanavijiji wanaoitumia hasa katika nyakati za dharura na ugonjwa.

3. Wawekezaji mbali mbali hushindwa kuwekeza katika sekta ya utalii hapa Zanzibar kutokana na urasimu uliopo nchini ambapo mamlaka ya ukuzaji vitega uchumi (ZIPA) imelalamikiwa kwa hilo. Hivyo, tunashauri Serikali iwe na dhamira ya dhati kukuza utalii kwa kuweka *One Stop Center* kwa ajili ya wawekezaji mbali mbali na hasa wa sekta ya utalii.

4. Mfumo wa vyama vingi vya michezo nchini wa kuwa Mweyekiti kutoka Unguja na Makamo wake kutoka Pemba umepitwa na wakati na unahitaji kubadilishwa kwani unakwamisha maendeleo ya michezo kwa upande wa Pemba.

5. Upatikanaji wa takwimu sahihi bado ni tatizo linaloathiri mipango ya utangazaji na uendelezaji utalii nchini

6. Kutokuwepo kwa walimu wa kutosha wenye viwango vya elimu vinavyotosheleza katika fani ya habari, uandishi, Utalii na huduma za mahoteli ni tatizo sugu la Wizara.

7. Uchache wa wataalamu katika Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC), mitambo na vifaa vipya pamoja na mafunzo kwa watendaji wa Shirika hilo bado hayakidhi haja ya kuingia kwenye teknolojia ya digitali ifikapo Disemba 2012. Aidha, uchache wa wataalamu pia ni tatizo sugu kwa Chuo cha Maendeleo ya Utalii cha Zanzibar.

2.6 MAPENDEKEZO YA KAMATI

1. Ni wajibu wa Wizara kupigania kwa nguvu zote kuyaondoa matatizo yanayorejesha nyuma maendeleo ya michezo nchini ambayo Kamati imeyasikia moja kwa moja kutoka kwa wanamichezo wenyewe yakiwemo:
    - Kukosekana ushirikiano baina ya taasisi na vilabu vya michezo vya Tanzania Bara na hapa Zanzibar, hususan kwenye michezo ya Kimataifa
    - Kukosekana ruzuku kwa wakati inapohitajika
    - Uvamizi wa viwanaja vya michezo na kuwakosesha vijana nafas za mazoezi
    - Kukosekana utaratibu mzuri wa Wizara kuendeleza sekta ya michezo kwa kutoelekeza vyema matumizi ya rasilimali watu, ambapo mafunzo ya michezo hupewa watendaji wasiohusika na michezo
    - Kutopatikana kwa motivations za kimichezo

- Kutopewa kipaumbele na Serikali kuu kwa kuondolewa utaratibu wa Mhe. Rais kuonana na wanamichezo kila baada ya muda maalum
- Kukosekana kwa jengo maalum la ofisi za wanamichezo kwa vyama vyote vilivyosajiliwa
- Kutokuwa na umoja na ubunifu baina ya viongozi wa vyama vya michezo
- Uongozi michezoni kugubikwa na rushwa na hatimaye wale wasiokuwa na uwezo wa kuongoza huchaguliwa kuwa ndio viongozi

Matatizo haya yakitafutiwa suluhisho ndiyo dawa ya kuinua hadhi ya Zanzibar kimichezo kama ilivyokuwa hapo zamani. Aidha, Kamati inapendekeza Michezo ipewe kipaumbele kwani kwa ulimwengu wa leo michezo ni ajira.

2. Wizara isaidie Baraza la Taifa la michezo la Zanzíbar kuanzisha miradi midogo midogo kwa ajili ya kujipatia fedha za kujiendesha badala ya kutegemea ruzuku pekee ambayo haikidhi haja ya kuviendeleza vilabu vyote nchini.
3. Kamati imeagiza Wizara kuwasilisha orodha za viwanja vya michezo kwa kila Wilaya ili kufuatilia ni viwanja gani vilivyovamiwa kwa matumizi mengine yakiwemo yale ya makaazi.
4. Ili kujenga ari ya wanamichezo wa Zanzibar na kuirejesha hadhi ya Zanzibar michezoni, Kamati imeishauri Wizara kuandaa utaratibu wa kuwapa tunzo za heshima wale waliowahi kulipatia hadhi Taifa letu kimichezo.
5. Kufuatia kuanza kwa taratibu za uajiri wa kudumu Hoteli ya Bwawani na kubainika baadhi ya mapungufu kwa baadhi ya wajiriwa, Kamati inaishauri Wizara ifikirie kiubinadamu zaidi mapungufu hayo na isiyafanye kuwa ndio msingi wa kutowaajiri wahusika hasa tukizingatia kuwa wameshapoteza nguvu zao nyingi kwa kuitumikia hoteli hiyo kwa mikataba ya miezi sita sita ambapo hawakua na haki yoyote.
6. Kamati imeishauri Wizara kuanzisha kampuni ya ulinzi na usalama ndani ya Hoteli ya Bwawani kwani ni jambo la kushangaza sana kwa hoteli kubwa kama hiyo kukosa huduma hiyo muhimu.
7. Kutokana na hali mbaya ya kudharauliwa kwa mahakama zetu pamoja na yale wanayoyatolea uamuzi, Kamati inaishauri Serikali kuunda "*Executive Argency"* ambayo itampa mamlaka Mkurugenzi wa Mashtaka kushughulikia mambo yote ya kisheria nchini, ikiwemo kufuatilia "orders" zinazotolewa na Mahakama ili kuzipa nguvu mahakama zetu kwa kutodharauliwa orders hizo.
8. Kwa vile Hoteli ya Bwawani ndio jicho la Serikali yetu, Kamati inaishauri Wizara ifanye hima kulirekebisha eneo lililomong'onyoka la ukingo wa hoteli ya Bwawani kwani kila wakichelewa nguvu za maji zinazidi kuteka eneo kubwa zaidi la ardhí.
9. Kamati inaiagiza Wizara kuipitia upya mikataba yote iliyofungwa kati yake na wateja, na wadaiwa sugu wote washughulikiwe kulingana na muongozo wa sheria.
10. Wizara iwe wazi katika kulizungumza suala la uwanachama wa Zanzibar *"Federation International Footbal Association*" (FIFA) kwamba halina mwelekeo tangu hapo mwanzo na hivyo hapakuwa nahaja ya kuwatia tamaa wananchi. Kamati inataka ijulishwe ni nani hasa anayestahiki kulizungumza suala hili mbele ya vyombo vya habari kwani kuna mtindo wa watu maarufu kutoa tarifa kuhusu jambo hilo.
11. Kamati inasisitiza kwamba utaratibu wa tenda ufuatwe ili kuiuza nyumba ya Shirika la Utalii ya Jambiani ambayo inaonekana kukumbwa na mmong'onyoko na kuwa katika mazingira yasiyopendeza kiutalii. Aidha, Kamati inaagiza kwamba, nyumba za Makunduchi zisiuzwe na badala yake zitumike kama chanzo cha mapato kwa shirika ili zichangie katika kujiendesha lenyewe.
12. Kutokana na hali ya ofisi ya bandari kuwa ndio waamuzi wakuu wa mambo yanayohusu bandarini, Kamati inaiomba Wizara kulifuatilia suala la ujenzi wa jengo jipya kwa ajili ya ofisi ya utalii ili kujua taratibu zao kama zinaruhusu ujenzi huo au wana mipango mengine.
13. Wizara iwe na utaratibu wa kuishirikisaha Kamati kwenye mambo yake. Kwa mfano: Kupokelewa kwa nyasi bandia za uwanja wa Gombani Waheshimiwa Wajumbe kwa upande wa Pemba wangealikwa na kuhudhuria ingeleta sura ya ushirikiano zaidi.

14. Wizara, kwa kushirikiana na redio binafsi zilizopo nchini wachukue hatua za ziada katika kuhakikisha matangazo ya redio za FM yanawafikia wananchi wote wa Unguja na Pemba kwani imebainika kuwa redio nyingi kati ya hazo haziwafikii wananchi wa Pemba.
15. Kamati imeitaka Wizara kuwasimamia vyema wamiliki wa redio binafsi nchini hususan wale wenye tabia ya kuwarekodi Waheshimiwa na wananchi mbalimbali bila ya ridhaa zao ili waache tabia hiyo, kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na maadili ya kazi yao.
16. Wizara ifanye mazungumzo na *"Zanzibar Electric Cooperation "*ZECO ili kuwapunguzia gharama za umeme kwa angalau asilimia hamsini wamiliki wa redio binafsi zinazojihusisha na ujenzi wa maadili sahihi ya Mzanzibari ili waweze kuendelea na shughuli zao hapa nchini.
17. Ili kukinusuru na kufungwa kabisa, na kuhamishiwa nchini Rwanda kituo cha EACROTANAL hakina budi kuendelezwa na kutatuliwa matatizo yanayokikabili ili kifufuliwe na kutumika kwa mujibu wa malengo yaliyopangwa. Kamati inashauri Serikali kuiongeza bajeti ya Kituo cha EACROTANAL kwa nia ya kutimiza azma hiyo.
18. Wizara ishirikiane na Wizara ya Mambo ya ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Idara ya Uhamiaji ili kuipatia Kamisheni ya Utalii takwimu sahihi za wageni wanaoingia nchini ili hatimaye Kamisheni iweze kupanga mipango yake kwa uhakika.
19. Wizara izitumie fursa za kisheria kwa watalii wanaohusishwa na kesi mbalimbali nchini kwa kuziingiza kesi hizo kwenye "*first truck cases*" ili ziweze kusikilizwa haraka kabla ya watalii hao kuondoka.
20. Kamisheni ya Utalii imeagizwa kuipitia upya sera ya utalii kwani imepitwa na wakati.
21. Kamati inahitaji taarifa rasmi za uhakika juu ya shutuma zinazokikumba chuo cha maendeleo ya utalii kilichopo Maruhubi.
22. Iko haja kwa Serikali kuwachunguza kwa kina mafundi wa kigeni wa mahoteli Pemba kwani baadhi yao hwenda kinyume na sheria za nchi kwa kufanya uvunaji wa mazao ya baharini.
23. Kamati imeliagiza Shirika la Utalii kuzirejesha hoteli za Wete na Mkoani mikononi mwa Serikali kwani hadi sasa mkodishwaji, kampuni ya National Marketing, imeshindwa kuziendeleza kwa namna yoyote ile.
24. Ni vyema taasisi za SMZ zinapokabidhiwa sehemu ya ardhi au jengo kwa ajili ya matumizi yao, zipatiwe hati miliki badala ya kupeana kwa mdomo tu kama ilivyozoeleka hivi sasa. Kamati ime muagiza Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupeleka maombi maalumu (special request) kwa Waziri wa Ardhi ili apatiwe hati miliki ya kisiwa cha Kuji kwa matumizi ya Shirika la Utalii.
25. Ili kuiondolea Kamisheni ya Utalii mzigo mzito wa kodi ya ofisi huko Pemba, Kamati imeitaka Wizara ilitafutie ufumbuzi suala la jengo la Kamisheni ya Utalii kwamba linafaa kunyanyuliwa ghorofa au laa kwani kwa muda mrefu halijashughulikiwa na hadi sasa tathmini inaonesha kuwa hwenda lisiweze tena kuhimili mikiki ya ghorofa.
26. Wizara inawajibika kuvifanyia tathmini vyama vvya michezo mara kwa mara ili kuyajua matatizo yanayovikabili. Aidha, katika kutatua suala la kukosekana ruzuku kwa vilabu vya michezo vya Pemba, Wizara iharakishe mpango wake mpya utakaoviwezesha vyama vya michezo kuomba na kupata ruzuku hiyo moja kwa moja kupitia mratibu wa michezo badala ya kupeleka maombi hayo kwa Katibu mtendaji wa BMTZ. Vile vile ruzuku za vyama zitolewe kwa vile vyama vyenye umoja na mshikamano wa kweli Kitaifa ili kuepusha kuvunjika moyo kwa wanamichezo wa Pemba.
27. Ili kuepusha msururu wa malalamiko kutoka vyama vya michezo nchini, Mwenyekiti na Katibu mtendaji wa Baraza wafanye baadhi ya maamuzi ya matumizi ya mwezi badala ya kusubiri kikao cha boda ambacho hufanyika kila baada ya miezi mitatu. Aidha, iko haja kwa Wizara kutoa nafasi maalum kwa michezo mengine badala ya mpira wa miguu pekee ili kuondosha dhana ya upendeleo kwa mpira wa miguu.
28. Kamati inaiomba kwa dhati SMZ kufuatilia kwa undani suala la nafasi ya Zanzíbar kwenye michezo ya Kimataifa kwani hadi sasa Zanzíbar inashirikishwa kama sehemu tu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ya kupewa fursa kama nchi nyengine huru, kwa hali hii Zanzíbar haiwezi kuinuka kimichezo. Aidha, baada ya mazungumzo na viongozi wa Baraza la Taifa la Michezo la Zanzíbar pamoja na viongozi wa vilabu vya michezo, Kamati imebaini kuwa utetezi wa Zanzíbar kama ni nchi kupitia Katiba mpya ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania ndio njia pekee itakayowapa nafasi vijana wa Kizanzibari kwenye michezo ya Kimataifa.

29. Licha ya kufungwa kwa mtambo (transmeter) kwa ajili ya matangazo ya dijitali ya televisheni, bado iko haja kubwa ya kuharakisha upatikanaji wa vifaa, mitambo na rasilimali watu itakayoiwezesha Zanzibar kuingia kikamilifu katika mfumo wa dijitali ifikapo tarehe 31 Disemba 2012. Aidha, Kamati imeliamuru Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kulipa deni lake haraka kwa Tume ya Utangazaji ili fedha hizo zipate kutumika kwa ajili ya mambo mengine yakiwemo yale ya taaluma na uhamasishaji wa wananchi juu ya umuhimu wa kutumia vifaa vya teknolojia ya digitali. Kadhalika, Kamati pia inapendekeza kutungwa Sheria ya kuzuia uingizwaji wa vifaa vya Analogi nchini kama njia moja ya kuwafanya wananchi waepukane na matumizi ya vifaa hivyo.
30. Wizara ichukue hatua za makusudi kuanzisha ofisi za Shirika la utalii Pemba kwani hadi wakati Kamati ilipofanya ziara yake ya mwisho mwishoni mwa mwaka 2011, Shirika halina ofisi wala mtendaji yeyote kwa upande wa Pemba.
31. Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kushirikiana na Wizara ya Kilimo na maliasili ili kuona kuwa mashirikiano ya karibu kati ya Kamisheni ya Utalii na uongozi wa Jozani yanapatikana, kwani kukosekana kwake kunaleta madhara kwa maendeleo ya utalii nchini kwa kukosekana mbinu bora za kuutangaza msitu wa Jozani kama kivutio cha utalii kimataifa.

    Katika suala zima la kuuendeleza utalii nchini, Kamati imewakumbusha viongozi wa hifadhi ya Jozani kuitumia vyema fursa ya kukusanya mapato waliyopewa na Serikali yao kwa kuweka akiba na kubuni miradi mikubwa ya kuuendeleza msitu wa jozani ili uzidi kuvutia watalii wengi zaidi.
32. Kutokana na ukosefu wa taaluma ya uandaaji na uandishi wa mpango kazi kwa vyama vingi vya michezo Pemba, Wizara kupitia Baraza la Taifa la Michezo la Zanzibar inawajibika kuwaandalia mafunzo hayo ili waweze kujipangia shughuli zao za mwaka na kufanya harakati mbali mbali zitakazowawezesha kupata ruzuku kwani kuwa na mpango kazi (action plan) ni moja ya sifa za kupatiwa ruzuku hiyo.
33. Wizara ifanye jitihada zaidi ya kuyahakiki maeneo yake ya kihistoria na kuyaepusha na kupoteza uhalisia wake kutokana na uvamizi wa ardhi.

SEHEMU YA TATU

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

3.1 UTANGULIZI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Wizara mpya iliyoanzishwa katika Serikali ya awamu ya saba ambayo ni sehemu tu ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Sekta ya mifugo na ile ya uvuvi ni tegemeo la idadi kubwa ya watu, hususan wale wanaoishi katika ukanda wa pwani, ikiwemo Zanzibar. Kwa msingi huo basi, Serikali imeamua kuunda Wizara maalumu itakayoshughulikia maendeleo ya mifugo na uvuvi kwa maslahi ya Taifa kwa ujumla.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inafanya kazi kupitia mgawanyo wa Idara zake sita ambazo ni:-

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
3. Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo
4. Idara ya Uzalishaji wa Mifugo.
5. Idara ya Mazao ya Baharini
6. Idara ya Maendeleo ya Uvuvi.

3.2 UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA – UNGUJA

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilijipangia malengo mbali mbali katika kutekeleza majukumu yake ya msingi. Utekelezaji halisi wa Wizara ni kama ifuatavyo:

1. Wafanyakazi 55 walipatiwa semina ya siku moja juu ya sheria za kazi, ajira, mahusiano kazini, afya na usalama kazini, ustawi wa jamii na fidia kwa wafanyakazi na sheria mpya ya utumishi wa umma kwa jumla.
2. Wafugaji 7,785 wametembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu juu ya wafugaji ikiwemo ufugaji wa kuku, mbuzi na ng'ombe. Vile vile vikundi 14 vya wafugaji vimetembelewa na kupatiwa taaluma ya ufugaji ikiwemo uimarishaji wa malisho, hifadhi ya malisho na ufugaji wa kuku wa kienyeji, chotara na kuku wa kabila za kigeni.
3. Mabango 100 juu ya kuhamasisha utumiaji wa bidhaa za mifugo zinazozalishwa nchini yametayarishwa na kusambazwa katika wilaya za Unguja. Aidha, vipeperushi 300 juu ya ufugaji wa sungura vimetayarishwa na kusambazwa kwa wananchi.
4. Jumla ya mitego 65,020 katika vijiji 12 ilikaguliwa na kuwekewa dawa katika wilaya 10 za Zanzibar.
5. Jumla ya doria 29 za mikoko zilifanyika kati ya doria 30 zilizopangwa na hekta 28 zilioteshwa mikoko.
6. Mafunzo ya siku mbili kuhusu uandishi wa mapendekezo ya miradi ulifanyika ambao jumla ya washiriki 25 kutoka Unguja na Pemba walihudhuria.
7. Vipindi vinne (4) vya redio na vinne (4) vya TV juu ya upandaji na uhifadhi wa malisho, utunzaji bora wa ndama na ufugaji wa kuku vimetayarishwa na urushaji wake umetekelezwa kwa asilimia 50.
8. Jumla ya ng'ombe 921 wamepandishwa kwa njia ya sindano.
9. Wapandishaji 10 wamepatiwa mafunzo ya upandishaji kwa njia ya sindano Pemba. Aidha matayarisho ya mafunzo kwa wapandishaji 15 wa Unguja yamekamilika na mafunzo yatafanyika mnamo robo ya tatu ya mwaka 2011/2012.
10. Bodi ya zabuni ya Wizara imekwishaanza taratibu zakutafuta mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa uzio (wire fence) katika kituo cha kuzalisha mbegu za majani bora kwa lishe ya mifugo cha Kizimbani.
11. Mradi wa MACEMP umeiwezesha Idara ya Misitu kwa matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa kuipatia Idara hiyo fedha za kutumikana kwa kuangamiza jumla ya kunguru 550,120 kati ya 1,200,000 waliopangiwa kuangamizwa. Aidha, sheria ndogo za uhifadhi kwa vijiji 12 zimeandaliwa ampapo taaluma juu ya sheria ndogo za uhifadhi wa vijiji 12 pia imetolewa.
12. Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeshakamilisha kuandika na kuipitisha Sera ya Mifugo. Sera hii imekwishapitiwa na wadau wa sekta husika na imekwishajadiliwa katika kikao cha Makatibu Wakuu imekwishapelekwa Baraza la Mapinduzi ambapo inatarajiwa kujadiliwa mapema katika kikao cha mwezi wa Januari 2012.
13. Mipango ya kuifanyia mapitio sheria dhidi ya ukatili wa wanyama inaendelea kwa mashirikiano ya wanasheria wa Wizara na taasisi husika kama, vile *"Zanzibar Animal Affection Society"* (ZAASO) na "*Zanzibar Society for Protection and Care of Animals"* (ZSPCA) zinazojihusisha na kupinga ukatili dhidi ya wanyama hapa nchini.
14. Wizara inaendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa mujibu wa mahitaji ya Taasisi za Wizara hii. Jumla ya wafanyakazi 65 wamesaidiwa kulipiwa mafunzo yao waliyopata ndani na nje ya nchi. Aidha wazalishaji wanajamii 18 (9 Unguja na 9 kutoka Pemba) walipelekwa nchini Uchina kuangalia na kusoma mbinu bora za uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini.

3.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

3.3.1 Mradi wa usimamizi wa mazingira ya baharí na ukanda wa pwani "*Marine and Coastal Environment Management Projec"* (MACEMP).

Huu ni mradi wa miaka sita kuanzia mwezi Disemba 2005 hadi Disemba 2011. Mradi huu hivi sasa uko katika kipindi chake cha mwisho.

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2011, mradi wa *Marine and Coastal Environment Management Project* (MACEMP) ulitekeleza yafuatayo:

1. Kuratibu kazi za mradi kwa kuwezesha utekelezaji wa kazi za kila siku ambapo mikutano 9 ya zabuni ilifanyika, watendaji 31 wamelipiwa ada za masomo, ununuzi wa stationery na mafuta lita 9,000 umefanyika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi pamoja na doria, safari za ndani 45 na za nje 8 zimefanyika kwa ajili ya kukagua kazi na kujifunza kwa kujionea. Mishahara kwa

wafanyakazi 34 imelipwa, kodi ya miezi 6 ya jengo pamoja na huduma za mawasiliano zimelipwa. Jumla ya seti 30 za viatu na makoti ya mvua yamenunuliwa na kupewa wafanyakazi husika, madereva 2 walipatiwa sare (*uniform*) na jumla ya piki piki 7 zilifanyiwa matengenezo.

2. Katika uhifadhi wa Mali Kale sehemu za kihistoria 19 (5 Unguja na 14 Pemba) zimefanyiwa ukarabatiwa,
3. Mkandarasi wa majengo mawili ya kihistoria ya (Beit al Ajaib na Peace Memorial Museum) amepatikana na majengo yameanza kukarabatiwa na kazi inaendelea.
4. Vikundi 8 vya wavuvi vimepatiwa mafunzo juu ya uvuvi wa kienyeji endelevu na vikundi 8 kutoka Shehia 8 za Wilaya ya Mkoani vimepatiwa mafunzo na kugharamiwa utendaji wa doria *Pemba Channel Conservation Area* (PECCA) ambapo jumla ya doria 6 zilifanyika.
5. Miradi ya kijamii midogo midogo iliendelea kuibuliwa na kwa kushirikiana na *Tanzania Social Action Fund* (TASAF) miradi iliyopatiwa fedha imefuatiliwa. Aidha, rasimu ya kwanza ya ripoti ya tathmini ya miradi ya jamii iliwasilishwa kwa *Marine and Coastal Environment Management Project* (MACEMP).
6. Sheria ndogo ndogo za shehia 20 za kanda ya ukanda wa pwani zimetengenezwa ili kuiwezesha Idara ya Mazingira kusimamia uhifadhi mazingira ya ukanda wa pwani kwa kuimarisha kamati za mazingira za Wilaya na Shehia.
7. Kwa kuandaa Sera ya Tawala za Mikoa na kusimamia ukamilishwaji wa mpango wa mafunzo (Training plan) ambapo rasimu ya mwanzo ya Sera ya Serikali za Mikoa imetayarishwa na imefanyiwa mapitio ili kuziwezesha Tawala za Mikoa katika usimamizi shirikishi wa rasilimali katika ngazi za mikoa. Aidha rasimu ya ripoti juu ya mpango wa mafunzo imekamilika na kuwasilishwa MACEMP.
8. Kuiwezesha Idara ya Ardhi na Mipango Miji kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi (land use plan) kwa kupitia mipango ya matumizi ardhi ambapo mipango 5 ya majaribio kwa vijiji vya ukanda wa pwani imeandaliwa na kukamilishwa kwa vijiji vya Makangale, Tondooni, Paje na Bwejuu. Aidha rasimu za ramani za mipango ya matumizi bora ya ardhi (land use plan) za Wilaya 10 zimeshaandaliwa.
9. Kuiwezesha Idara ya Misitu kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa kuangamiza kunguru ambapo jumla ya kunguru 550,120 kati ya 1,200,000 waliangamizwa. Aidha, mradi umesaidia kuandaa sheria ndogo ndogo za uhifadhi kwa vijiji 12 ambapo ilitolewa taaluma juu ya sheria ndogo za uhifadhi.
10. Jumla ya mitego 65,020 katika vijiji 12 ilikaguliwa na kuwekewa dawa ya kuangamiza inzi wanaoharibu embe katika Wilaya 10 za Zanzibar
11. Jumla ya doria 30 za mikoko zilipangwa kufanywa ambapo jumla ya doria 29 zilifanyika na jumla ya hekta 28 za mikoko zilioteshwa.
12. Kusaidia Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu katika usimamizi na uendelezaji kazi za uvuvi na uhifadhi katika bahari kuu.
13. Vijiji 17 vimetembelewa na kukaguliwa takwimu za uvuvi ili kuimarisha upatikananji wa taarifa za uvuvi.
14. Mratibu wa Global Environment Facility (GEF) alifanya ziara mnamo mwezi Oktoba 2011 kutembelea mradi ili kufuatilia maendeleo ya mradi yaliyopatikana. Aidha ujumbe wa Ufatiliaji toka Benki ya Dunia ulitembelea mradi na kufanya tathmini ya mradi mnamo mwezi Novemba 2011.
15. Utaratibu wa kumpata mshauri mwelekezi kuhusu Mpango wa Ushauri wa Uongozi wa Utalii (Consultancy Service on Tourism Management Plan) umekamilika na ripoti imewasilishwa.
16. Jumla ya miradi 317 ya jamii (147 Unguja na 170 Pemba) imefuatiliwa na rasimu ya mwanzo ya ripoti imewasilishwa MACEMP.

3.3.2 Mradi wa kudhibiti kichaa cha mbwa.

Mradi huu ni kutokomeza kichaa cha mbwa nchini.Mradi umeanza Unguja Agosti 2005 chini ya ufadhili wa shirika la "*World Society for Protection of Animals* (WSPA)". Pemba, mradi wenye lengo hilo hilo umeanza mwaka 2010 kwa msaada wa shirika la "*Melinda and Bill Gate Foundation".*

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2011, mradi wa kudhibiti kichaa cha mbwa ulitekeleza yafuatayo:

1. Jumla ya Mbwa 169 wamefungwa uzazi

2. Jumla ya Mbwa 4,575 walipatiwa dawa za minyoo.
3. Jumla ya Mbwa 1,417 walioogeshwa ili kuwakinga na maradhi yanayotokana na kupe.
4. Jumla ya Paka 286 waliofungwa uzazi.
5. Jumla ya Paka 659 walipatiwa chanjo ya kichaa cha Mbwa.
6. Jumla ya Punda 506 walitibiwa kutokana na maradhi ya aina mbali mbali.
7. Jumla ya Ng'ombe 317 wa gari walitibiwa kutokana na maradhi ya aina mbali mbali.
8. Jumla ya Mbuzi 875 walitibiwa kutokana na maradhi ya aina mbali mbali.
9. Jumla ya Mbwa 3,887 walipatiwa chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa.
10. Jumla ya Mbwa 486 walitibiwa kutokana na maradhi ya aina mbali mbali.

3.3.3 Mradi wa kudhibiti mafua ya ndege na Nguruwe.

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kudhibiti maradhi ya Mafua makali ya ndege ambapo Wizara imepania kudhibiti maradhi haya yasiingie nchini na kutuwezesha kukabiliana nayo pindi yakiingia.
Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2011, mradi wa kudhibiti kichaa cha mbwa ulitekeleza yafuatayo:

1. Vifaa vya maabara kama vile Air-conditions 2 zimenunuliwa pamoja na kutia grills katika madirisha ya maabara na kupaka rangi kwa ajili ya kurahisisha uchunguzi wa maradhi.
2. Uchunguzi wa kimaabara kwa kuku 50 kutoka masoko ya Mwanakwerekwe na Darajani umefanyika ambapo matokeo yake yameonesha kuwa hakuna kuku alieathirika na ugonjwa wa Mafua makali ya ndege.

3.3.4 Mradi wa kupandisha ng'ombe kwa sindano (Artificial Insemination)

Mradi huu una madhumuni ya kuzalisha ng'ombe chotara wenye uzalishaji mzuri wa maziwa ambao wataongeza kipato cha wafugaji wadogo wadogo na kuwapunguzia umasikini.
Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2011, mradi wa kupandisha ng'ombe kwa sindano ulitekeleza yafuatayo:

1. Madume ya mbegu yaliendelea kutunzawa kwa kupewa mahitaji muhimu ikiwa ni pamoja na malisho, maji na chakula cha ziada.
2. Jumla ya mirija 234 imezalishwa na mirija 400 imenunuliwa kwa kusambazwa kwa ajili ya kazi za upandishaji ng'ombe kwa sindano Unguja na Pemba.
3. Jumla ya ng'ombe 921 wamepandishwa kwa njia ya sindano.
4. Mtambo wa gesi ya "*liquid nitrogen*" uliopo Maruhubi umefanyiwa matengenezo kwa kushirikiana na mtaalamu kutoka Kenya ambaye ameletwa na kampuni iliyofunga mtambo huo.
5. Lita 7,694 za "liquid Nitrogen" zimezalishwa na kusambazwa Unguja na Pemba.
6. Eneo la kituo cha Upandishaji wa Ng'ombe kwa Sindano limekwisha kupimwa na kuwekewa alama (Bicons). Aidha utaratibu wa kupitisha utoaji wa zabuni ya ujenzi zinaendelea.
7. Wapandishaji 10 wamepatiwa mafunzo Pemba. Aidha matayarisho ya mafunzo kwa wapandishaji 15 wa Unguja yamekamilika na mafunzo yatafanyika robo ya tatu.

3.3.5 Mradi wa Miundombinu na Huduma za Mifugo

Mradi wa miundombinu na huduma za mifugo una lengo la kukarabati miundo mbinu ya mifugo iliopo pamoja na kuiboresha ili ikidhi haja iliyowekwa.
Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2011, mradi wa miundombinu na huduma za mifugo ulitekeleza yafuatayo:

1. Eneo linalodhamiriwa kujenga chinjio huko Kisakasaka limekwishatengwa na kukaguliwa.
2. Matayarisho ya kuandaa michoro kwa njia ya zabuni yamefanyika kwa kufanya kazi ya kutayarisha TORs za mchoro wa chinjio. TOR imejadiliwa na kufanyiwa marekebisho na kukubaliwa na Bodi ya Zabuni.

3.4 UTEKELEZAJI WA WIZARA KWA UPANDE WA PEMBA

Kwa kipindi cha Julai/Septemba 2011**,** Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

1. Kununua kompyuta na imeanza kutumiwa kwa **k**azi za kuweka kumbukumbu za wafanyakazi kwenye kompyuta. Hii itasaidia kurahisisha upatikanaji wa habarí za uhakika za wafanyakazi. Aidha, Idara iliweza kununua kompyuta ikijumuisha printer, antivirus na flash disks kwa matumizi ya Ofisi.

2. Wizara imefanikiwa kununua Vespa ambayo inatumika kwa kazi za idara ya mipango, sera na utafiti ikiwa ni pamoja na kufuatilia shughuli mbali mbali za Miradi na kazi kwa ujumla.

3. Wizara imefanikiwa kuendesha mafunzo ya Ukimwi na Jinsia kwa wanakamati wa Wizara hii.

4. Mafunzo msasa ya siku 12 yalitolewa kwa watoa huduma za awali za Utabibu wa mifugo (Community Animal Health Workers) 33 kama ifuatavyo:

WILAYA	**IDADI**	**SHEHIA WALIZOTOKEA**
Micheweni	7	Majenzi Micheweni, Njuguni, Chimba, Mgogoni, Kinyasini, Kifundi, Makangale.
Wete	8	Pandani, Kizimbani, Kiungoni, Ukunjwi Fundo, Shengejuu, chwale, Mtambwe Kusini.
Chake Chake	8	Pujini Dodo, Mfikiwa, Ng'ambwa, Vitongoji, Wesha, Shungi na Chonga.
Mkoani	10	Kengeja, Makombeni, Ukutini, Mkanyageni, Mizingani, Kiwani, Chumbageni, Mtangani, Kangani, Kisiwapanza.
JUMLA	**33**	

Jumla ya mifugo 177,318 ilipewa chanjo dhidi ya magonjwa mbali mbali kama ifuatavyo:-

WANYAMA	**WALIOKINGWA**				**JUMLA**
	M'weni	**Wete**	**Chake**	**Mkoani**	
Mbwa	0	14	64	0	78
Paka	0	0	10	0	10
Kuku	648	104,000	43,586	28,996	177,230
JUMLA	**648**	**104,014**	**43,660**	**28,996**	**177,318**

5. Jumla ya majogoo 80 ya mbegu yatokanayo na utafiti shirikishi yaligaiwa kwa wafugaji

6. Kikundi cha wafugaji 20 wa ng'ombe wa maziwa wa shehia ya Kifundi walipewa mafunzo juu ya utunzaji bora wa ng'ombe wa maziwa na walitembelea wafugaji wenzao wa Uchozini ambako walijifunza jinsi ya kupanda majani . Pia kikundi cha wafugaji 21 wa mbuzi wa kijiji cha Jombwe Muambe walipatiwa mafunzo juu ya utunzaji bora wa mbuzi wa maziwa na walitembelea wafugaji wenzao wa shehia ya Chokocho ili kujifunza zaidi

7. Jumla ya wafugaji 1,982 walipatiwa ushauri wa kitaalamu juu ya ufugaji bora wa ng'ombe, mbuzi na kuku kupitia maafisa ugani katika wilaya zote za Pemba.

8. Jumla ya n'gombe 355 walipandishwa kwa sindano wakiwemo Chotara 278 na wa asili 77.

9. Ununuzi wa madawa kwa shamba la Chamanangwe ulifanyika na ng'ombe 19 waliopo shambani walipatiwa tiba ya minyoo

10. Pikipiki moja mpya ilinunuliwa na kukabidhiwa kwa Afisa mifugo Wilaya ya Chake chake.

11. Mfugaji wa Mabata wa Pandani (Kwamwewe) alitembelewa na kupewa ushauri wa ufugaji bora wa mabata.

12. Kwa kupitia mradi wa *Agriculture Support Development Project – Livestock* (ASDP-L) Idara iliendelea na kazi ya kutoa taaluma ya ufugaji bora wa ng'ombe, mbuzi na kuku kupitia skuli 152 za wafugaji (farmer field school) ndani ya shehia 40 za Pemba.

13. Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ilifanikiwa kufanya mikutano minne (4) Lengo la mikutano hiyo ilizungumzia zaidi juu ya Wavuvi kuhusu kuhakikisha kila mvuvi ni lazima awe na leseni ya uvuvi na chombo kwa wale wenye kumiliki vyombo vya Uvuvi.

14. Sambamba na hilo Idara ilifanya kazi ya kuendelea kuwafafanulia Wavuvi sheria ya Uvuvi na kutanabahisha wavuvi ambao hawana leseni watashitakiwa kwa mujibu wa sheria. Mikutano hii imefanywa kwa mashirikiano kati ya Afisi Kuu ya Idara, Maafisa Uvuvi Wilaya, Masheha wa shehia husika na wenyeviti wa kamati za Uvuvi kwenye shehia hizo.

15. Jumla ya mifugo 23,353 ilipewa kinga dhidi ya wadudu mbali mbali wanaoathiri mifugo kama ifuatavyo:-

WANYAMA	**WALIOKINGWA**				**JUMLA**
	M'weni	**Wete**	**Chake**	**Mkoani**	
Ng'ombe	4,732	6,717	2,794	2,717	16,960
Mbuzi	1,731	1,918	803	3,134	5,786
Kuku	7	0	51	313	371
Mbwa	16	30	20	71	137
Paka	18	7	4	28	57
Punda	2	0	9	31	42
JUMLA	**6,505**	**8,672**	**3,681**	**6,294**	**23,353**

3.5 UTEKELEZAJI WA AHADI ZA WIZARA

Hadi kufikia Disemba 2010, Wizara imeweza kutekeleza ahadi zake zilizotolewa katika Baraza la Wawakilishi katika mkutano wa Bajeti 2010/2011 kama ifuatavyo;-

1. Kuanzisha utafiti shirikishi wa kuku katika kupata kuku wanaokuwa haraka, wanaotaga zaidi na wanaostahamili maradhi.

   Kwa kushirikiana na mradi wa *Agriculture Support Services Programme* (ASSP/ASDPL), utafiti shirikishi unafanyika kwa mfugaji binafsi wa kuku ambaye anazalisha majogoo na kuyasambaza kwa wafugaji kupandishia kuku wa kienyeji kwa lengo la kupata kuku chotara wanaokuwa haraka, wanaotaga zaidi na wanaostahamili maradhi ukilinganisha na kuku wa kigeni (layers and broilers).

2. Kuendelea na mazungumzo na wawekezaji kwa kuyaendeleza mashamba ya Chamanangwe na Magome

   Kwa upande wa shamba la Chamanangwe, wawekezaji kutoka Dubai walilitembelea lakini hadi sasa hawajatoa kauli rasmi ya kuwekeza. Pamoja na hayo, idara ya uzalishaji wa mifugo inaendelea kuliendeleza kwa kuanzisha kituo cha utafiti wa mifugo. Kazi za utafiti zitafanyika rasmi katika mwaka ujao wa fedha 2012/2013.
   Aidha, idara ya uzalishaji mifugo imeanzisha kituo cha kutoa huduma za utibabu na uzalishaji wa mifugo katika shamba la Magome ili kuwasogezea wananchi huduma za wafugaji wao.

3. Kushajiisha ufugaji kuku wa kisasa kwa mashirikiano baina ya wawekezaji wa ndani na wafugaji wenyewe ili kuongeza uzalishaji wa ndani wa mayai na nyama.

Kwa kupitia mradi wa ASSP/ASDP-L ushajiishaji unafanyika kwa kupitia skuli za wafugaji (farmers field schools) ambazo zimeenea katika shehia 40 za Pemba. Aidha, ushajiishaji hufanywa pia kwa kupitia Jumuiya ya wafugaji *Poultry Farmers Development Organisation* (POFADEO) na LIFSOPE kwa njia ya mikutano na makongamano.

4. Kutoa elimu kwa wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini kwa kuwapeleka vijana 30 nchini China kwa ajili ya mafunzo hayo

Mnamo tarehe 26 Agosti hadi tarehe 26 Septemba, 2011 vijana 30 kutoka shehia mbalimbali za Unguja na Pemba walifanya ziara ya kimafunzo nchini China. Wizara inaendelea na kazi ya kuwaendeleza vijana hao ili waweze kuitumia elimu waliyoipata kwenye mafunzo hayo kwa maslahi yao na Taifa kwa ujumla.

5. Kutatua matatizo yanayojitokeza katika madiko ya wavuvi

Wizara kupitia idara ya maendeleo ya uvuvi na kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wameweza kutatua mgogoro wa wavuvi wa shehia ya Kichuani iliopo katika Wilaya ya Chake chake Pemba.

6. Kujenga josho la ng'ombe la kwanza katika Wilaya ya Mkoani

Wizara imefanikiwa kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa josho hilo ambalo ni Mjimbini na limethibitishwa na wataalamu kwamba ni eneo linalofaa kwa kazi hiyo. Aidha, jitihada za kulipatia hati miliki zimeanza kufanywa na tayari Wizara husika imelikagua eneo hilo.

7. Kuanzishwa eneo la karantini Pemba

Wizara imekwisha fanya malipo Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati ili kulipima eneo la Nziwengi na kutoa hati miliki ili eneo hilo liwe sehemu ya karanti huko Pemba.

3.6 MATUMIZI YA FEDHA

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 11,628,445,000/=, kati ya hizo shilingi 2,089,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 9,539,445,000/= kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Aidha, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,020,000,000/= kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.

Kamati ilijuulishwa kuwa hadi kufikia mwezi wa Disemba 2011, jumla ya shilingi 1,308,952,517.00 tayari zimeshatumika, zikiwa ni shilingi 876,393,517.00 kwa ajili ya mishahara na maposho na shilingi 432,559,000.00 kwa matumizi mengineyo.

3.7 CHANGAMOTO

1. Mwamko mdogo wa sheria katika jamii zetu hupelekea kukwamisha suala zima la kutetea haki za wanyama.
2. Ufinyu wa Bajeti unapelekea kusuasua kwa malengo ya Wizara kwani mbali na bajeti kuwa ngodo, uingizwaji wa fedha zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi haukuwa wa kuridhisha.
3. Upungufu wa vitendea kazi vya kutosha katika kufanikisha shughuli za miradi ya Wizara.
4. Kutosikika vizuri kwa Redio ya Shirika la Utangazaji Zanzíbar katika baadhi ya sehemu ya Zanzibar inapelekea kwa baadhi ya wafugaji kukosa kupata taarifa za huduma mapema, hivyo hukwamisha shughuli kwani ni redio pekee wanayotumia wakulima kwa kutoa matangazo.
5. Kupitwa na wakati kwa Sheria nyingi za mifugo ambako kunapelekea wananchi kuzivunja kwamakusudi.

3.8 MAPENDEKEZO YA KAMATI

1. Wizara ifanye jitihada za makusudi ili kuhakikisha kwamba inatafuta soko kwa ajili ya gesi ya ziada inayozalishwa kwenye kituo cha A1 ili kunyanyua kipato chao na kuongeza ufanisi wa kazi zao.

2. Elimu ya ufugaji, utunzaji pamoja na biashara ya samaki inahitajika, hususan kwa wananchi wanaoanzisha mabwawa ya ufugaji wa samaki na chaza. i.e wafugaji wengi mfano Bumbwini makoba hupata hasara kubwa.
3. Wizara ilichukulie hatua suala la kiwanda cha sukari kumwaga taka za sumu kwenye mto na kuathiri mabwawa ya ufugaji wa samaki, kama taarifa ya huko makoba ilivyoeleza.
4. Wizara ifanye juhudi za kuhakikisha inapatiwa kibali cha kuajiri vijana 20 zaidi, ili wawe ni wafanyakazi wa kudumu katika chinjio la Kisakasaka, kwa kumuandikia barua rasmi katibu mkuu wa Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuwasilisha kopi ya barua hiyo kwa kamati.
5. Kutokana na utata wa umiliki wa jengo la chinjio la Kisakasaka kati ya Wizara, wananchi na mmiliki binafsi, ni vyema Wizara ikatafuta hati halali ya jengo ili kujiepusha na migogoro ambayo inaweza kutokea hapo baadae.
   Pamoja na mpango wa Wizara wa kujenga chinjio jipya ambalo litagharimu shilingi milioni 224 katika bajeti ya mwaka huu, Kamati imeshauri kuanzishwa kwa machinjio ya zoni ili kuondoa usumbufu wanaoupata wananchi kwa hivi sasa.
6. Kamati ilipokea taarifa kwamba, suala la uvuvi wa bahari kuu bado halina Sheria hapa nchini na hivyo, linaendeshwa kwa makubaliano tu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Ingawa Sheria kama hiyo ipo Tanzania Bara, bado haijaridhiwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutumika Zanzíbar kwani imegundulika kuwa inahitaji kufanyiwa marekebisho ili kusibu mazingira ya Zanzibar. Hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iitazame mikataba na makubaliano yote yanayofikiwa kwa mtazamo wa mbele ili kuiepusha Zanzibar na maafa yanayoweza kuepukika.
7. Ili kuifanya miradi ya mifugo na uvuvi kuleta tija kwa wananchi wetu, Wizara iunde Tume ya wataalamu ambayo itakuwa na kazi kuu ya kufanya tathmini ya miradi kama ni ya manufaa au laa kabla ya mradi wowote kuanza. Aidha, Kamati inashauri vikundi vya miradi viundwe kwa kuzingatia watu wenye fani zinazowiyana na wapatiwe miradi muwafaka kwa fani zao ili kupata maendeleo yanayohitajika.
8. Kutokana na taarifa kwamba kiwanda cha samaki hakifanyi kazi kwani Wizara ya fedha imempa mwekezaji ambaye hana uwezo wa kuzalisha samaki hao. Hivyo, Wizara imeijuulisha Wizara ya Fedha kuwepo kwa mwekezaji mpya mzalendo ambaye analihitaji eneo hilo. Kinachosubiriwa ni kufutwa Kibali cha Mwanzo na kutolewa Kibali kipya kwa mwekezaji huyo mpya. Ni matarajio ya Kamati yetu kwamba Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo itafanya uamuzi wa busara kwa haraka iwezekanavyo ili kuendeleza sekta hii ya uvuvi nchini. Wizara inategemea baada ya miezi 6 viwanda vya samaki vitaanza kuonekana nchini.
9. Wizara kwa kushirikiana na Serikali kuu ilitizame kwa kina ombi la wanakamati wa masoko ya Matemwe na Pwani Mchangani la kupatiwa boti za uokozi, hasa kwa kulikumbuka tukio la ajali lililoikumba nchi yetu hivi karibuni.
   Aidha, Wizara pia ifikirie njia za kuwapatia vijana wa maeneo ya ukanda wa pwani mafunzo ya kuogelea na uokozi kwa kadiri uwezo utakavyoruhusu.
10. Kamati imeishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara kuandaa mpango wa kuwalinda wazalishaji wadogo wadogo wa mazao ya mifugo na uvuvi (protectionism policy) ili kuwaepusha na uvamizi wa wafanyabiashara kutoka nje na kupelekea kuanguka wazalendo kibiashara.
11. Wizara ifanye upembuzi yakinifu ili kujua bei halisi ya mwani kwenye soko la dunia pamoja na gharama zote wanazozipata makampuni ya mwani tangu ununuzi, usafirishaji mpaka kuuzwa kwake ili kwa kushirikiana na makampuni yenyewe, waweze kutoa bei yenye maslahi kwa pande zote mbili.
    Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha miundombinu kwenye vijiji 75 vinavyozalisha mwani pamoja na kuingilia kati mpango mzima wa ununuzi na uuzaji wa mwani kwa kuanzisha Shirika la kusimamia upangaji wa bei na uuzwaji wa mwani kama ilivyo kwa zao la karafuu ili kuchangia kwenye pato la Taifa.
12. Ni vyema Wizara ikaandaa utaratibu wa kuwaongoza wakulima wa mwani kwa kila Wilaya ili kuwajengea ari zaidi na uwezo wa kuzalisha kwa kiwango kikubwa ambacho kitakidhi mahitaji yao ya kimaisha.

13. Wizara imeshauriwa kutafuta misaada mbalimbali kwa nia ya kuwatoa wavuvi kwenye uvuvi wa kale na kufikia uvuvi wa kisasa wenye kuleta tija zaidi. Mafunzo maalumu ya matumizi ya fedha na vifaa yatolewe kabla ya misaada na misaada hiyo itolewe kwa wakati unapohitajika.
15. Kamati inatoa wito kwa viongozi na wanasiasa nchini, kutoingilia kati ugawaji wa vifaa vya misaada ya uvuvi kwani kufanya hivyo ni kukwamisha ugawaji uliopangwa na huathiri matumizi
17. Kutokana na umuhimu wa huduma za ushauri na utibabu wa mifugo, Wizara haina budi kujenga jengo lao wenyewe badala ya kuendelea kulitegemea jengo la hivi sasa lililopo Dunga ambalo ni chakavu sana na haliko kwenye miliki yao.
18. Wizara inakabiliwa na tatizo la upungufu mkubwa wa watendaji hususan katika Idara ya utibabu wa mifugo Pemba ambayo ina mfanyakazi mmoja tu hadi kufikia Disemba 2011.
19. Kamati imeishauri Wizara kutoa taaluma ya jinsi ya kuchagua mradi kwa jamii kabla wanajamii hao hawajaingia kwenye miradi ili kuwajengea uwezo wa kuibua miradi yenye tija.
20. Ni vyema Wizara kuibua miradi mikubwa ambayo italeta faida ya muda mrefu kwa jamii kwani miradi mingi tuliyonayo hivi sasa ni mifupi mifupi na ambayo hukabiliwa na tatizo la upungufu wa wataalamu wa kuitenda.
21. Wizara inahitaji kujipanga kikamilifu kwa kuwaandaa vijana wetu wa Kizanzibari kwenye fani zote zinazohitajika kwenye uzalishaji bora wa mazao ya baharini kabla ya hatua ya kuanzishwa rasmi kiwanda cha samaki hapa Zanzibar ili kuepusha utegemezi wa wataalamu kutoka nje ya nchi ambao hulipwa fedha nyingi sana.
22. Jitihada za makusudi zinahitajika kuelimisha jamii ya wafugaji wa kuku hasa wa kienyeji umuhimu wa kuwafikisha vituoni kila wanapougua, badala ya hatua zinazochukuliwa sasa za kuwachinja tu.

SEHEMU YA NNE.

WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA USHIRIKA

4.1 UTANGULIZI

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi kiuchumi na Ushirika ni Wizara mpya katika Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar ya awamu ya saba, yenye muundo wa umoja wa Kitaifa. Wizara hii imeundwa rasmi Novemba 2010, ikiwa na jukumu Kubwa la kusimamia shughuli zote za kuongeza ajira kwa vijana na kuinua hali zao na taifa kwa ujumla. Kimuundo, Wizara ina Idara saba, Kamisheni moja na Afisi kuu Pemba kama ifuatavyo:-

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
3. Idara ya Maendeleo ya Ushirika
4. Idara ya Mikopo
5. Idara ya Uratibu wa Miradi na Sekta za kiuchumi
6. Kamisheni ya Kazi
7. Idara ya Ajira
8. Idara ya Usalama na Afya Kazini
9. Afisi Kuu Pemba

4.2 UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA – UNGUJA

Kamati ilipata fursa ya kukagua na kupata taarifa ya utendaji halisi wa majukumu ya msingi ya Wizara ya Kazi. Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa kipindi cha Julai/ Disemba 2011, ambapo utekelezaji halisi ulikuwa kama ifuatavyo:

4.2.1 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Katika kipindi cha Julai/Disemba, Idara imetekeleza mambo yafuatayo:

- Katika kipindi hicho pia Idara imesimamia uandaaji wa Mpango Mkakati wa Wizara kwa miaka mitatu (2011/12 – 2013/14) pamoja na Mpango wa Mafunzo kwa watendaji. Mpango Mkakati ndio muongozo mkuu wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha mwaka 2011/12 hadi 2013/14.
- Jumla ya mapendekezo ya miradi saba kuhusiana na utekelezaji wa MKUZA II yameandaliwa. Miradi mitano inahusiana na utekelezaji wa Klasta ya 1 ya UKUZAJI UCHUMI NA UPUNGUZAJI UMASKINI WA KIPATO na miradi miwili ni kwa utekelezaji wa Klasta ya 3 ya UTAWALA BORA NA UMOJA WA KITAIFA. Miradi ya Klasta ya 1 ni; 'Zanzibar Community Economic Empowerment Programme'; 'Capacity Support for the Ministry of Labour'; 'Employment Promotion Programme'; 'Cooperative Reform Project' na 'SACCOS Enhancement Project'; Miradi inayohusiana na utekelezaji wa Klasta ya 3 ya MKUZA II ni; Labour Law Enhancement na Strengthening of Occupational Safety and Health Inspection System of Workplaces in Zanzibar.
- Kamati ya masuala mtambuka imeundwa baada ya hadidu rejea kupitiwa na kuthibitishwa na Kamati Tendaji ya Wizara. Kazi hiyo imefanywa kwa kushirikiana na taasisi husika zinazoratibu masuala mtambuka ambazo ni Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Afisi ya Rais,Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- Mafunzo ya kuaandaa Mpango Kazi yamefanyika. Jumla ya watendaji 16 wa idara zilizo chini ya Wizara hii wamepatiwa mafunzo hayo na tayari wameanza kuutumia mfumo uliowasilishwa katika uandaaji wa Mpango Kazi. Mafunzo hayo yamesaidia kuandaa mpango kazi kwa ufanisi.
- Katika juhudi za kuwaelimisha wahusika mbalimbali juu ya Sera ya Ajira, Wizara imefanya mkutano wa kuiwasilisha Sera hiyo ili iweze kueleweka vizuri na kutekelezwa.
- Katika kutayarisha Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Kamati ya wataalamu inayojumuisha sekta mbalimbali imeundwa .Hadidu rejea za Mtaalamu wa kuongoza utaratibu wa kuandaa sera zimeandaliwa na kupitishwa kwenye kamati ya Wataalamu. Kamati hiyo imepewa jukumu la kukusanya taarifa za awali (taarifa kuhusu kilimo, elimu, mazingira na biashara). Mazungumzo na *International Labour Organisation* (ILO) yameshafanyika ili kupatikana Mtaalamu Elekezi wa kusaidia kuandaa sera hiyo.
- Katika kuwasilisha na kufuatilia maombi ya miradi, mazungumzo na washirika wa maendeleo yamefanyika kwa baadhi ya miradi iliyoandaliwa. Mazungumzo hayo yamefanywa kwa washirika wafuatao: IFAD, (MIVARFP- 'Marketing Infrastructure ,Value Additional and Rural Finance Programme), Save the Children (Programme on the elimination of Child Labour), ILO "*Youth Employment Facility" (*YEP) na "*United Nations Assisstance Programme"* (UNDAP).
- Maombi kwa ajili ya Mtaalamu wa kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini yamewasilishwa ILO kwa hatua za kutafuta Mshauri elekezi kufanya kazi hiyo.
- Katika kuimarisha mashirikiano na Wizara husika za Tanzania Bara, Wizara imefanya mazungumzo ya ana kwa ana na watendaji wa Wizara washirika za Tanzania Bara na kukubaliana kuhusu maeneo ya mashirikano na taratibu za uendeshaji wa mikutano ya mashirikiano.Wizara zinazohusika ni Wizara ya Kazi na Ajira,Wizara ya kilimo,Usalama wa Chakula na Ushirika na Afisi ya Waziri Mkuu,Uwekezaji na Uwezeshaji. Rasimu ya Mkataba wa Makubaliano *"Memorundum of Understanding"* (MOU) inafanyiwa kazi ili uridhiwe na pande zote mbili ikiwa kama ni muongozo wa mashirikiano.
- Rasimu ya mwisho ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika imekamilika baada ya kupitishwa katika vikao mbalimbali ikiwemo Kamati Tendaji ya Wizara. Rasimu hiyo imepangwa kuwasilishwa kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu katika mwezi wa Machi 2012.
- Wizara imefanya tafiti katika maeneo muhimu ya kiuchumi ili kubaini fursa zilizopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Miradi kadhaa imeibuliwa na kuandikiwa ikiwemo mradi wa kilimo cha umwagiliaji maji (Gando), ufugaji kuku (Piki), Ufugaji nyuki-asali (Vitongoji), mradi wa kuimarisha bidhaa zinazotokana na maziwa zikiwemo siagi na samli (Kisiwani kwa Binti Abedi), uzalishaji na usindikaji wa viungo (Mtambwe).

4.2.2 Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Wizara imetoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi 55 kuhusiana na sheria na kanuni za utumishi wa umma iliyotolewa kwa kada ya madereva, wahudumu, walinzi, na watunzaji masjala. Pia mafunzo yamefanyika kwa watendaji 30 kwa lengo la kujenga mashirikiano na mtandao wa kazi, kufanya kazi

kwa pamoja na ushawishi wa kupenda kazi kwa kujituma. Mafunzo hayo yamefanywa kwa kushirikiana na Asasi isiyo ya kiserikali "*Business Development Service Providrs"* (BDS Provider) ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya uwezeshaji. Aidha Wafanyakazi 2 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi (mwanamke 1 na mwanamme1), katika fani ya *"Human Resource Management"* HRM - China na Udereva Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam.

Wizara imewapatia wafanyakazi watatu mafunzo ya muda mfupi, kati ya hao wanawake wawili katika fani ya Human Resource "*Eastern and Southern African Management Institute*" (ESAMI) Dar es salaam na mwanamme mmoja katika fani ya Record Management katika chuo cha Utumishi wa Umma-Zanzibar. Pia Wizara imelipia gharama za masomo kwa wafanyakazi wanne wakiwemo wanaume watatu na mwanamke mmoja wanaosomea fani za Uhasibu, Sheria, na Usalama wa Afya kazini.

Wizara imefanya matayarisho ya ujenzi wa ofisi kwa kuandaa michoro na makisio ya gharama za ujenzi. Mawasiliano yamefanywa na Wizara ya Majenzi ili kufanya tathmini ya jengo na kutoa ushauri wa kitaalamu.

4.2.3 Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Katika kipindi cha Julai - Disemba, 2011, Idara hii imetekeleza mambo makuu yafuatayo:-

Wajasiriamali 34 wamepatiwa mafunzo ya siku tatu, kuhusu ujasiriamali, kuweka kumbukumbu na kujenga mtandao wa biashara ili kutanua soko. Mafunzo hayo yalisaidia kuwajengea uwezo wajasiriamali na baadhi yao mafunzo yaliwahamasisha kushiriki katika mashindano ya Mama Shujaa wa Chakula wa Tanzania na wengine katika maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa gharama zao. Aidha mafunzo ya ujasiriamali kwa wananchi 30 wa mikoa miwili ya Pemba na Unguja yametolewa. Mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha kusimamia na kuendesha biashara zao.

Vipeperushi 10,000 vimetolewa kwa kushirikiana na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ili kuhamasisha wananchi kuhifadhi benki na kuwekeza katika miradi endelevu ya kiuchumi fedha zao zinazotokana na mauzo ya karafuu.

Imeandaa mapendekezo matano ya miradi ambayo ni Mradi wa Kutayarisha Mfumo wa Taarifa (Data Base) za wajasiriamali, Mradi wa Kukuza Vipaji vya Ubunifu kwa Wajasiriamali, Mradi wa Kampeni ya Ushajihishaji wa Utamaduni wa Kiujasiriamali na Mradi wa Utoaji Huduma za Kibiashara kwa Wajasiriamali.

Hatua za awali za kukusanya taarifa za kiuchumi na kijamii zimefanywa katika maeneo yaliyoteuliwa kuwa vijiji vya mfano ili kushajihisha utafutaji wa rasilimali kwa kuviwezesha kiuchumi vijiji hivyo. Dodoso kwa ajili ya kukusanya taarifa hizo limeshaandaliwa na taarifa kamili za vijiji vya Mbuyu Tende - Unguja na Ungi - Pemba vilivyoteuliwa kuwa vijiji vya mfano zitatolewa baada ya kazi hiyo kukamilika.

4.4.4 Idara ya Mikopo

Idara hii ina jukumu la kusimamia utoaji mikopo nafuu ili kuwawezesha wananchi kiuchumi na kupunguza umasikini. Lengo ni kuwawezesha wananchi waweze kujiajiri na kujipatia kipato halali na endelevu ili kumudu maisha yao. Kwa kipindi cha Julai/ Disemba 2011, Idara imetekeleza yafuatayo:

Kwa kushirikiana na Benki ya Watu wa Zanzibar hadi kufikia mwezi Disemba 2011 jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Kumi na Sita, Mia Tisa na Arobaini (Tshs 1,516,940,000/=) zimetolewa kupitia mfuko wa JK/AK**.** Changamoto iliyopo ni kwamba utoaji wa fedha za mikopo kupitia mfuko wa JK/AK unaosimamiwa na Benki ya watu wa Zanzibar kwa sasa hauendi kwa kasi inayotarajiwa.

Aidha Idara ya mikopo kupitia Mfuko wa Kujitegemea imetoa mikopo yenye thamani ya Tshs 70,500,000/= kwa mikopo 108 Unguja na Pemba.

Katika ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo jumla ya Tshs 59,555,300/= zimerejeshwa kwa Unguja na Pemba katika Mfuko wa Kujitegemea . Kwa upande wa mfuko wa JK/AK jumla ya Tshs 26,377,831.78 zimerejeshwa kwa Unguja na Pemba. Marejesho ya mfuko wa JK/AK yanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo Benki kuwasubiri wateja badala ya kufuatilia marejesho ya mikopo.

Katika kupitia taratibu za mikopo ili kurahisisha utoaji na urejeshwaji mikopo Idara ilifanya mikutano na masheha , viongozi wa Wilaya na Wajumbe wa Kamati ya Uwezeshaji za Wilaya kuwafahamisha utaratibu mpya wa mikopo na majukumu yao katika suala zima la utoaji na ufuatiliaji mikopo . Pia kwa kushirikiana na Benki ya Watu wa Zanzibar Idara ilifanya mafunzo yaliyogharimu Tshs 6,028,000/= yalifanyika kwa Wilaya zote isipokuwa Wilaya ya Mjini Magharibi. Mafunzo kwa wilaya ya Mjini Magharibi yamepangwa kufanyika hapo baadae.

Mfanyakazi mmoja mwanamke amegharamiwa kufanya mafunzo ya muda mrefu katika fani ya uhasibu, ngazi ya "Post Graduate Diploma "Chuo cha Fedha *"Institute of Financial Management"* (IFM) Dar es Salaam. Aidha Mfanyakazi mmoja mwanamme amegharamiwa kufanya mafunzo ya muda mfupi katika ngazi ya cheti, fani ya rasilimali watu katika matawi ya DAR COLLEGE yalioko Pemba.

4.4.5 Idara ya Maendeleo ya Ushirika

Idara hii ina jukumu la kuihamasisha jamii kujiunga na vyama vya ushirika, kusimamia uundwaji wa vyama hivyo pamoja na kuviendeleza na kuvijengea uwezo.
Katika kipindi cha Julai - Disemba, 2011, Idara hii imetekeleza mambo makuu yafuatayo:-

- Vijana 1,398 wameshajihishwa kuanzisha vikundi vya miradi ya kiuchumi kwenye Shehia za Mwambe Mkoani, Uwandani, Chake Chake na Maziwa Ngombe Micheweni kwa Pemba na katika Shehia za Uzini Chumbuni, Kikwajuni na Kisiwandui kwa Unguja. Aidha jumla ya vijana 1,526 wameshajihishwa kuanzisha miradi ya kiuchumi kupitia vyama vya ushirika. Pia vikundi (165 Unguja; na 104 Pemba) vimehamasishwa kuanzisha miradi ya kiuchumi.

- Vyama 3 vimeandikiwa miradi yenye thamani ya Tshs 58,850,000/. Vyama hivyo ni Shirikisho la Vyama vya Ushirika Zanzibar – "*Cooperative Union of Zanzibar"* (CUZA) (Tshs 44, 000,000/-), Ushirika wa Ulezi Una Kazi uliopo Fujoni (Tshs 7,400,000/-) na Ushirika wa Tunakuona ulioko Bumbwini (Tshs 7,450,000/-). Maombi hayo yameshapita mchujo wa kwanza kwenye Shirika la Foundation for Civil Societies Dar Es Salaam na hatua zaidi zinaendelea kwa ajiliya kupata ufadhili.

- Jumla ya vyama 346 vya Wilaya tatu za Mkoani -Pemba, Mjini na Kusini - Unguja vimehakikiwa kati ya vyama 1,682 vilivyosajiliwa. Ukaguzi unaonesha kuwa vyama 1,336 vilivyosajiliwa vimekufa. Aidha vyama 366 (182 Wilaya za Magharibi na 184 Micheweni) vimehakikiwa.

- Jumla ya vikundi 109 (51 Unguja na 58 Pemba) vimepatiwa taaluma ya mwanzo ya kuwaandaa kujua misingi na taratibu za kuanzisha vyama imara vya ushirika. Pia vikundi hivyo vimewezeshwa kuandaa sheria ndogondogo na kuchagua uongozi wa awali wa kusimamia shughuli za usajili wa vyama hivyo. SACCOS 6 na vyama vya uzalishaji mali 103 (51 Unguja na 58 Pemba) vimepata sheria ndogo ndogo.

- Idara ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imefanya ukaguzi kwa vyama 26 zikiwemo SACCOS 24 na vyama 2 vya uzalishaji kwa Unguja. Pia watendaji 15 walipata mafunzo ya ukaguzi kati ya hao watendaji 5 kutoka kitengo cha ukaguzi na 10 kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.

- Idara imetoa mafunzo kwa viongozi 30 kutoka SACCOS 15 zilizomo Wilaya ya magharibi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuzimudu na kuziendesha SACCOS zao kwa ufanisi

zaidi. Aidha mafunzo ya vitendo yametolewa kwa wanachama na viongozi 1,959. (W'ke 1,326 na Wanaume 633) kutoka vyama 130 Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalihusu uendeshaji wa SACCOS, utunzaji wa hesabu, utawala bora na uongozi wa vyama vya ushirika.

- Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), mfumo wa kompyuta wa ufuatiliaji na uchambuzi wa shughuli za ushirika (Computerized Cooperative Monitoring and Analysis system "COCOMAS") umeanzishwa na umefanyiwa majaribio kwa Wilaya za Magharibi – Unguja na Micheweni - Pemba.
- Idara imeimarisha mashirikiano kwa washirika wa maendeleo "*Cooperative Rural Development Bank"* (CRDB), ILO, wawakilishi wa vyama vikuu (CUZA na ZASCU) na, Wizara ya Kilimo (ASSP na MIVARP). Pia Idara imepatiwa mafunzo kwa watendaji wake kupitia mashirika ya ACTION AIDS na ACRA na mafunzo ya ziara ya Nairobi na Mkoa wa Kilimanjaro kwa viongozi wa Wizara.

4.4.6 Kamisheni ya Kazi

Katika kipindi cha Julai/Disemba 2011, Kamisheni ya Kazi imetekeleza mambo yafuatayo

- Kamisheni ya Kazi imeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya masuala yanayohusiana na mambo ya kazi. Vipindi viwili vya Redio vilirushwa hewani na kurejewa kila mwezi kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar . Aidha maafisa kazi wa kitengo cha elimu kazi wamezitembelea jumla ya taasisi 2 kwa lengo la kutoa elimu kwa njia ya majadiliano ya ana kwa ana kati ya waajiri na waajiriwa. Utoaji huu wa elimu unasaidia katika kutoa taaluma juu ya sheria za kazi na utekelezaji wake ili waajiri na wafanyakazi waweze kutekeleza majukumu na wajibu wao ipaswavyo.
- Imeendelea na hatua za kuziweka vyema Sheria na Kanuni za kazi hasa zinazohusu utatuzi wa migogoro ya Kazi. Kanuni mbili za sheria za kazi ikiwemo Kanuni ya Kamati ya Utatu na Kanuni ya usuluhishi na Uamuzi wa migogoro ya Kazi zimeshafanywa na kuridhiwa na kikao cha Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi.
- Katika jitihada za kuimarisha masuala ya Utatu (tripartism), Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi imeundwa na kuanza kazi zake. Bodi hii inaundwa na wajumbe kutoka Serikalini (wajumbe 4), Jumuiya ya Waajiri Zanzibar – "*Zanzibar Employers Association"* ZANEMA (wajumbe 3) na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Zanzibar – *"Zanzibar Trade Union Congress"* (ZATUC) (wajumbe 3). Bodi hii ndio chombo cha kisheria kilichopewa mamlaka ya kuishauri Serikali kupitia Waziri wa Kazi juu ya mambo mbalimbali yanayohusu masuala ya kazi kwa hapa Zanzibar. Kuwepo kwa Bodi hii kutasaidia kuimarisha mahusiano mema kati ya Serikali na washirika wengine katika mambo ya kazi na kuondoa malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa washirika hao juu ya kutokuwepo kwa Bodi hii.
- Ukaguzi kazi umeendelea kufanywa katika taasisi mbalimbali za kazi. Jumla ya tasisi 37 zimefanyiwa ukaguzi kazi, ikijumuisha taasisi 23 za Unguja na taasisi 14 kwa upande wa Pemba. Kwa zile taasisi ambazo zilionekana kuwa na kasoro, miongozo imetolewa na kuziagiza kurekebisha kasoro hizo. Aidha kwa baadhi ya waajiri walioonekana kuwa sugu na kutokufuata miongozo inayotolewa na Serikali , hatua za kinidhamu zimechukuliwa dhidi yao ikiwemo kuwafutia vibali vya kufanya kazi. Mfano ni mfanyakazi wa kigeni wa Hoteli ya Neptune ambaye pamoja na kuonywa mara kadhaa juu ya tabia yake mbaya ya kuwadhalilisha wafanyakazi hususan wa kike aliendelea na tabia yake hiyo, hivyo kupelekea Kamishna wa Kazi kumfutia kibali chake cha kufanya kazi nchini. Hatua hizi zitasaidia katika kuwakumbusha waajiri na waajiriwa juu ya wajibu wao wa kufuata sheria zinazoongoza mambo ya Kazi hapa Zanzibar.

- Imetatua malalamiko yanayohusu mambo ya kazi ambapo jumla ya malalamiko 36 yalipokelewa, kati ya hayo malalamiko 27 yamepatiwa ufumbuzi , malalamiko 6 bado yanaendelea kufanyiwa kazi na malalamiko 3 yamepelekwa Mahakama ya Kazi kwa hatua zaidi. Kwa upande wa Pemba hakuna mgogoro ulioripotiwa katika kipindi hichi.

- Kamisheni ya Kazi imeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya masuala yanayohusiana na mambo ya kazi. Vipindi viwili vya Redio vilirushwa hewani na kurejewa kila mwezi kupitia Shirika la

Utangazaji la Zanzibar . Aidha maafisa kazi wa kitengo cha elimu kazi wamezitembelea jumla ya taasisi 2 kwa lengo la kutoa elimu kwa njia ya majadiliano ya ana kwa ana kati ya waajiri na waajiriwa. Utoaji huu wa elimu unasaidia kutekeleza majukumu na wajibu wao ipaswavyo.

4.4.7 Idara ya Ajira

Katika kipindi cha 2011/2012, Idara hii imetekeleza yafuatayo:
Baadhi ya taasisi zimeshaandikiwa barua za kuwasilisha taarifa za wafanyakazi wao waliowaajiri. Pia Wizara imeandaa dodoso la kukusanya taarifa za ajira katika ngazi ya Shehia ambapo imefanya mikutano na masheha wa Shehia 84 za Mkoa wa Mjini Magharibi kwa lengo la kuwafahamisha kuhusu zoezi la ukusanyaji wa taarifa hizo.Taarifa hizo zimeshaanza kuwasilishwa katika Ofisi za Wilaya.

Wizara imefanya mikutano miwili ya kamati za uzalishaji ajira kwa ngazi ya Mkoa kwa Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa kusini Pemba na mikutano mitano kwa ngazi ya Wilaya kwa wilaya za Chake Chake na Mkoani kwa Pemba na Magharibi kwa Unguja. Katika Mikutano hiyo wajumbe walielekezwa juu ya Sera ya Ajira , programu ya uzalishaji ajira na wajibu wa Kamati hizo.

Kupitia kituo cha kukusanya taarifa za soko la ajira Wizara imeorodhesha vijana 231 wanaotafuta ajira kwa lengo la kuwaunganisha na waajiri. Idara imewasaidia vijana 26 kupata ajira katika hoteli za kitalii, kati ya hao 16 wakiwa ni wanaume na 10 wanawake.
Mkurugenzi ajira na maafisa wawili wa Idara walifanya ziara ya mafunzo katika Wizara za Tanzania Bara kwa kutembelea Idara ya Ajira na Wakala wa Ajira ili kujifunza utekelezaji wa majukumu yao pamoja na kukubaliana maeneo ya mashirikiano.

Idara imefanya mkutano na Maafisa uajiri wa Taasisi 35 za sekta binafsi kwa kuzungumzia utekelezaji wa Sera ya Ajira na umuhimu wake katika kuwaajiri Wazanzibari kwa mujibu wa sera hiyo na Sera ya Vitega Uchumi.

Idara ilipata fursa ya kuhudhuria mkutano wa UTATU ulioitishwa na Shirikisho la vyama vya wafanyakazi Afrika Mashariki *"East African Trade Union Congress"* (EATUC) uliofanyika Rwanda na mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Mradi wa INTRA-ACP uliojadili itifaki ya soko la pamoja Afrika Mashariki na masuala ya uhamiaji.

4.4.8 Idara ya Usalama na Afya Kazini

Katika kipindi cha Julai/Disemba 2011, Idara hii imetekeleza yafuatayo:

- Sehemu 127 za kazi (105 Unguja na 22 Pemba) zimekaguliwa kwa kuangalia hali ya usalama na afya kwenye maeneo ya kazi.

- Mfanyakazi mmoja amepatiwa mafunzo juu ya mfumo wa ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za usajili wa sehemu za kazi katika mamlaka ya Usalama na Afya, Dar es salaam. Pia mfanyakazi mmoja amepelekwa masomoni kwa mafunzo ya shahada ya juu katika fani ya Usalama na Afya kazini kwenye chuo cha ILO kilichopo, Turin Italy. Aidha Wakaguzi 10 wa Usalama na Afya Kazini wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu za kisasa za ukaguzi.

- Wizara imezikaguwa na kuzitambua sehemu za kazi zilizosajiliwa na ZRB, Halmashauri za Wilaya, Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji na Mrajis Mkuu wa Serikali.

- Wizara imehudhuria mkutano wa kuweka viwango na miongozo inayohusu Ukimwi na TB kulingana na Usalama na Afya kazini kwenye sekta za mahotelini kwa nchi za Afrika Mashariki.

- Ziara ya kujifunza imefanyika katika Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini, Makao Makuu Dar es Salaam. Katika ziara hiyo pande mbili zimekubaliana kuendeleza mashirikiano yakiwemo wataalamu katika masuala ya ukaguzi wa usalama na afya kazini.

- Wizara imefanya ufuatiliaji na uchunguzi wa ajali za kuungua kwa Hoteli ya Matemwe Beach Village na kuzama kwa Meli ya MV Spice Islanders I. Taarifa zilizoandaliwa kutokana na ufuatiliaji huo zinatumika kufanya marekebisho kwenye taasisi husika na nyengine ili kukinga madhara ya aina hiyo yasitokee tena.

4.3 UTEKELEZAJI WA KAZI KWA UPANDE WA PEMBA

Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi ilifanya ziara ya kikazi Pemba na kuikagua Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kuanzia tarehe 12/12/2011 hadi tarehe 13/12/2011. Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini utekelezaji wa kazi za Wizara ulikuwa kama ifuatavyo:-

4.3.1 Idara ya Maendeleo yaVyama vya Ushurika

Katika kipindi cha Julai/Septemba 2011, Idara imesajili jumla ya vyama vya ushirika 102 kati ya vyama 60 vilivyojipangia kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Kama inavyoonekana kiwilaya;

WILAYA	CHAKE CHAKE	MKOANI	WETE	MICHEWENI	JUMLA
JUMLA	**28**	**33**	**33**	**8**	**102**

Hivyo inaifanya Idara ya ushirika kuwa na jumla ya vyama vya Ushirika 1,991 kama ifuatavyo-:

WILAYA	CHAKE CHAKE	MKOANI	WETE	MICHEWENI	JUMLA
JUMLA	**644**	**486**	**592**	**269**	**1,991**

Aidha utayarishaji wa Data base kwa vyama vya ushirika umekamilika kwa wilaya ya Micheweni. Jumla ya shehia ishirini na saba (27) zilifanyiwa kazi kukamilisha kasoro za ukusanyaji wa taarifa kwa vyama vilivyobakia.
Katika zoezi hilo jumla ya vyama 265 vilitarajiwa kuhakikiwa, 210 ndio vilivyohakikiwa na 182 kuonekana vipo hai.

Vilevile Idara imeweza kuzalisha ajira 1,100 kupitia vikundi 102 vya uzalishaji vilivyapatiwa usajili wa kudumu.
Idara pia imefanikiwa kuvikagua vyama vya ushirika 4 na kuvifungia mahesabu. Vyama hivyo ni “Hakiba Haiozi”, “Shikamana Saccos”, “Mpaji ni Mungu” na “Sebu Shari”.

4.3.2 Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Idara imefanikiswa kuendesha mafunzo kwa wajasiriamali 30 kwa wilaya zote za Pemba ikijumuisha makundi matatu (Wenye Kuishi na virusi vya UKIMWI, Walemavu na Wajasiriamali wa kawaida)

Idara pia imefanikisha kuandaa na kuendesha mikutano ya kamati za uwezeshaji wananchi kiuchumi za Wilaya ya Chake Chake na Mkoani. Kwa upande wa Wilaya za mkoa wa kaskazini inatarajiwa kufanyika hivi karibuni.

4.3.3 Idara ya Mikopo

Jumla ya mikopo 25 yenye thamani ya Tshs. 12,000,000/= imetolewa kwa watu binafsi katika shehia mbali mbali za Wilaya nne za Pemba.

Shughuli ya ufuatiliji urejeshaji wa mikopo ulifanyika ambapo jumla ya Tshs **12,064,000/=** zimekusanywa ikiwa ni marejesho ya Mikopo.

Idara inaendeleza utaratibu wake wa kutoa mikopo kwa awamu nne kwa mwaka (robo mwaka), sambamba na kukuza mashirikiano yake na Benki ya Zanzibar (PBZ), katika kuratibu mikopo ya AK/JK, pia Idara imefanya marekebisho makubwa ya fomu za maombi ya mikopo kwa mifuko yote inayoisimamia yaani AK/JK na Mfuko wa Kujitegemea.)

Vile vile Idara ya mikopo Pemba imeweza kupokea Vespa mpya moja kwa ajili ya kazi za ufuatiliaji wa mikopo pamoja na shughuli nyengine za ofisi

4.3.4 Kamisheni ya Kazi

Kutoa elimu juu ya Sheria za kazi ili wananchi waweze kuzifahamu sheria za kazi na kujua haki zao za msingi za kazi ni jukumu la Kamisheni ya Kazi. Katika kipindi cha miezi mitatu Julai – Septemba 2011 Kamisheni ya Kazi imetoa elimu juu ya kazi kwa taasisi tano.

Taasisi hizo ni MECCO, Sharouk Guest House, GAPCO, Zanea Sea Weed na GIM Sea weed.

Katika kipindi cha … 2011/2012 Kamisheni ya Kazi imefanikiwa kuzifanyia ukaguzi jumla ya taasisi 14 za sekta binafsi lengo ikiwa ni kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi. Kati ya taasisi hizo 8 ni kutoka Mkoa wa Kaskazini na 6 ni kutoka Mkoa wa Kusini Pemba**.**

4.3.5 Idara ya Usalama Kazini

.

Idara iliweza kuzifanyia ukaguzi taasisi kumi kati ya hizo taasisi sita ni za Mkoa wa Kusini na taasisi nne ni za Mkoa Kaskazini- Pemba.

Taasisi ambazo zimefanyiwa ukaguzi kwa-Mkoa wa Kusini Pemba ni Baraza la Mji Chake, Kampuni ya ujenzi ya Rans Ltd iliopo Shamiani Chake Chake, Fundu Lagon Hotel- Wambaa, Kampuni ya ujenzi wa barabara PRRP Wambaa, Le-tervan Hotel – Chake Chake, Ghala la mwani Machomane Chake Chake. Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, taasisi zilizopfanyiwa ukaguzi ni Baraza la Mji –Wete, MECCO Company Ltd – Wete, Farouk Guest House –Wete, Pemba Crown Hotel –Wete.

Mambo ambayo yaliangaliwa katika taasisi hizo ni Usafi wa Mazingira, Vifaa vya Kinga kwa wafanyakazi, Kinga za mashine, Vifaa vya huduma ya kwanza (First Aid kit), Ukaguzi wa Afya za wafanyakazi, Vifaa vya zimamoto, Hifadhi za umeme.

Katika ukaguzi huo inaonesha kwamba sehemu nyingi za kazi wafanyakazi hawana vifaa vya kinga kama vile glaves, mask, viatu na n.k) pamoja na ukaguzi wa afya za wafanyakazi wao.
Vilie vile idara imebaini kukosekana kwa vifaa vya zima moto pamoja na vya huduma ya kwanza (First Aid Kit).
Sehemu ambazo zimeonesha kukithiri changamoto hizo ni Mabaraza ya Mji (Wete, Chake Chake, na Mkoani), Mradi wa barabara PRRP, na Kwareni – Vitongoji pamoja na Mwambe.

4.4 MATUMIZI YA FEDHA

Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imetengewa jumla ya T. Shs 1,545,000,0000/= kwa kazi za kawaida, ambapo kati ya hizo, Shilingi za Kitanzania 465,000,000/= ni kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamiii na posho za wafanyakazi na zilizobaki (T.Shs. 1,080,000,0000/=) ni kwa matumizi mengineyo. Vile vile, jumla ya Shilingi za Kitanzania 90, 000, 0000/= zimetengwa kwa kazi za maendeleo.

Pia Wizara imepangiwa kukusanya mapato ya T. Shs. 68,500,000/= kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kupitia Kamisheni ya Kazi na Idara ya Maendeleo ya Ushirika.

Kamati imearifiwa kwamba, hadi kufikia mwezi Disemba 2011, Wizara imeingiziwa jumla ya T. Shs. 864,548,800/=, ambapo kati ya hizo, Shilingi za Kitanzania 431,493,215/= ni kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamiii na posho za wafanyakazi na Shilingi za Kitanzania 433,055,595/= ni kwa matumizi mengineyo.

Fedha zilizopatikana kwa matumizi mengineyo ni sawa na asilimia 40 ya makisio kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Kwa upande wa fedha za maendeleo, Wizara imeingiziwa jumla ya Shilingi za Kitanzania 30,000,000/= ambayo ni sawa na asilimia 33.3 ya kiwango kilichopangwa kwa mwaka 2011/12. Aidha, Wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi za Kitanzania 79,187,125/= sawa na asilimia 115 ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2011/12.

4.5 CHANGAMOTO

Katika utekelezaji wa shughuli zake, Wizara inakabiliwa na changamoto kuu zifuatazo:

- Ufinyu wa bajeti;
- Ukosefu wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi;
- Uhaba wa nafasi za Ofisi;
- Uwezo mdogo wa ujuzi miongoni mwa vijana, hali inayoathiri uwezo wao wa kuajirika kulingana na mahitaji ya soko la ajira;
- Ukosefu wa eneo la kufanyia kazi na kuuza bidhaa za wajasiriamali;
- Namna ya kuiimarisha sekta binafsi na sekta isiyorasmi ili ziweze kuzalisha nafasi zaidi za ajira;
- Matumaini makubwa ya wananchi ya kuwezeshwa kiuchumi ukilinganisha na uwezo uliopo;
- Ufinyu wa nyenzo na vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za ukaguzi wa hali ya afya na usalama katika sehemu za kazi na kufuatialia shughuli nyengine za Wizara;
- Mahitaji makubwa ya kuvifufua na kuviimarisha vyama vya ushirika ili viweze kuleta tija na kukidhi mahitaji ya wanachama wake.
- Ukosefu wa jengo la ofisi kwa upande wa Pemba.
- Ukosefu wa elimu inayokwenda na wakati kwa baadhi ya wafanyakazi.
- Tatizo la urejeshwaji wa mikopo kwa wakati.
- Uhaba wa wafanyakazi kwa baadhi ya maidara unaopelekea kuzorota kwa kazi.
- Kukosekana kwa utamaduni wa ujasiriamali katika jamii ya Wazanzibari.
- Kuibuka kwa vikundi vingi vinavyoundwa kisiasa kila ikikaribia wakati wa uchaguzi.

4.7 MAPENDEKEZO YA KAMATI

1. Wizara iwapatie mafunzo maalumu wajasiriamali wa Zanzibar juu ya umalizaji wa kazi zao (finishing) ili ziwe na mvuto na kupata soko la ndani na nje ya nchi.

2. Ili kuufanya mfuko wa AK na JK kuwa ni tegemeo la wananchi wanyonge na bila ya kupunguza kiwango cha utendaji cha Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ), Kamati inashauri mpango wa kuurejesha mfuko huu kwenye usimamizi wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika umalizwe kwa haraka.

3. Kamati imeitaka Wizara kuvipa kipaumbele maalumu vikundi vya watu wenye ulemavu katika kuwapatia mafunzo na mikopo ili waweze kujikwamua kwenye janga la utegemezi.

4. Katika jitihada za kupunguza unyanyasaji wa waajiriwa hasa wa sekta za binafsi, Kamati imeishauri Wizara kuwapa taarifa ya moja kwa moja wafanyakazi kupitia Wilaya zao kila yanapofanywa marekebisho ya mishahara.

5. Wizara ifanye kila njia ili kumuendeleza mjasiriamali Bwana Said pamoja na wale wote watakaojitokeza kuwa na ubunifu kama wake wa kuvumbua vitu vipya ambavyo ni chachu ya ujenzi wa njia mpya za uzalishaji na ukuwaji wa sekta ya viwanda hapa nchini. Ni wajibu wetu Wizara kupanga mipango ya muda mrefu kwa kushirikiana na Serikali kuu ili kuwa na muendelezo mzuri kwa vijana wetu wazalendo wenye mwelekeo kama huu. Aidha, ni vyema Wizara ikainunua gari hiyo ya Bwana Said na kuiweka makumbusho. Halkadhalika, Wizara isimamie suala zima la usajili wa karakana ya Bwana Said (SUGU) ili nayo itambulike Kitaifa.

6. Katika suala zima la utoaji na ufuatiliaji wa mikopo nchini, ni vyema Wizara ikawa na kitengo imara cha kuelimisha watendaji wa Serikali na wananchi wengine ili waelewe jinsi ya kupata mikopo na njia sahihi za matumizi ya mikopo hiyo kwa nia ya kujikwamua kutokana na janga la umasikini wa kipato.

7. Wafanyakazi wengi wa kada ya mahoteli hukosa haki zao za msingi kutoka kwa waajiri wao hasa mara baada ya kufukuzwa kazi, zoezi ambalo huwakumba mara kwa mara kutoka hoteli moja hadi nyengine. Tunatoa wito kwa Wizara kuwachukulia hatua waajiri wote wenye tabia ya unyanyasaji kwa waajiriwa.

8. Wizara, kwa kushirikiana na Serikali kuu haina budi kujenga Afisi maalumu kwa ajili ya Idara ya mikopo ili kuokoa fedha nyingi zinazotumika kwa kukodi majengo ambapo zaidi ya milioni 3.6 zinatumika kwa kulipia kodi kila mwaka kwa afisi za Unguja na Pemba. Kufanya hivyo, kutawasaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya matumizi mengine ya uendeshaji kama vile usafiri na kulipa stahiki za wafanyakazi wa idara hii, ili kuwajengea ari zaidi ya kuwajibika.

9. Idara ya mikopo inawajibu wa kufanya uhamasishaji maalumu wa uchukuaji na utumiaji mzuri wa
mikopo kwa akinamama, kwani pamoja na kuwa na asilimia ndogo ya fumgu la ukopaji, bado wanaonekana kutokuwa tayari na mikopo hiyo kwa kukopa asilimia 33 tu ya wakopaji wote ingawa wao ndio wengi kwa mahesabu ya idadi ya watu.

10. Kutokana na ukweli kwamba wadaiwa walio wengi hawalipi madeni yao, wakati umefika kwa Wizara kuandaa sheria ya kuwatia hatiani na kuwaadhibu wale wote watakaobainika kutolipa mikopo hiyo au kuichelewesha kwa makusudi.

11. Kamati inashauri Idara hii ya mikopo iendeshwe kwa utaratibu wa kuwa na bodi amabyo itafanya maamuzi yake ya msingi kwa utendaji bora zaidi.

12. Katika kusimamia vyema fedha za umma, ni jukumu la Wizara, kuanzisha data base ya wakopaji ambayo itaunganisha wakopaji wote kupitia taasisi mbalimbali za utoaji mikopo za Serikali na binafsi ili kuwaepusha na mikopo mingi kwa wakati mmoja ambayo hatimaye huwashinda kulipa.

13. Kutokana na idadi kubwa ya mifuko ya mikopo kwa wananchi, Kamati inakubaliana na wazo la kuunganisha mifuko yote yenye lengo moja la kumuinua mwananchi na kuwa ni mfuko mmoja tu ili kupata urahisi wa kufuatilia hasa tukitilia maanani kuwa tuna upungufu wa wafanyakazi wa kufuatilia mikopo hiyo.

14. Kamati inatoa agizo kwa Wizara kufuatilia hadi kujua taarifa sahihi kuhusu gari iliyotolewa na SMZ kwa ajili ya Idara ya mikopo na ambayo hadi sasa inatumiwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto.

15. Wizara ifanye jitihada za makusudi za kuongeza idadi ya wafanya kazi katika Idara ya mikopo ili kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa mikopo.

16. Kamati, kwa kushirikiana na Wizara inaomba Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais iwajibike ipaswavyo kuyakusanya mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi, kupitia kwenye hutuba zao Barazani kuyapeleka Serikalini ili yafanyiwe kazi kwa nia ya kuimarisha nchi yetu na watu wake.